# UKOMBOZI WA MWANAMKE KATIKA RIWAYA ZA HABWE

Na

MAOBE O. JACOB

C50/75903/2009

**Kazi hii imewasilishwa kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili (M.A) Kiswahili katika Chuo Kikuu Cha Nairobi.**

University of NAIROBI Library

0532230 0

JUNI 2011

## UNGAMO

Hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote kile.

2/11/2011 ……………………………… ………………………………

Tarehe. Maobe Omabene Jacob.

Kazi hii imetolewa Kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu Cha Nairobi.

3/11/2011 ……………………………… ………………………………

Tarehe. Dkt. Mwenda Mbatiah.

03-12-2011 ……………………………… ………………………………

Tarehe. Dkt. Omboga Zaja.

## SHUKRANI


Utafiti huu umekamilika kwa juhudi kubwa na mchango wa watu wengi. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na afya njema.

Shukrani za dhati kwa wasimamizi wangu Dkt. Mwenda Mbatiah na Dkt. Omboga Zaja kwa ushauri wenu na uvumilivu mlionipa wakati wa kuandika kazi hii. Mola azidi kuwabariki daima.

Shukrani za kipekee Ziwaendee wahadhiri wangu wa idara ya Isimu na Lugha wafuatao: Prof. Abdulaziz, Prof. Mberia, Prof. Habwe, Prof.Wamitila, Dkt. Rayya, Dkt. Buregeya, Dkt. Olali, Dkt. Kineene na Bw. Mungani. Wengine ni Dkt.Schroeder Dkt. Mkhwana, Bw. Mogambi , Dkt. Mbuthia na Dkt. Iribe. Utafiti huu haungewezekana bila juhudi zenu.

Nawashukuru wasimamizi na wahudumu wote wa Idara ya Isimu na Lugha kwa msaada ambao wamenipa. Mungu awajalie neema zake.

Shukrani za moyo wangu nampa mke wangu Norah Bochere kwa mapenzi na uvumilivu na himizo alizonipa nilipokuwa karibu kuvunjika moyo. Mungu aendelee kukupa uzima. Kwa Wanangu, Peninnah, Naomi, Askah, Hezron, Risper, Jemimmah na Sarange nasema ahsanteni kwa uvumilivu wenu.

Shukrani za dhati nawapokeza wanafunzi wenzangu: Dada Martha Owino, Peter Thamu, Hannington Gitonga, Paul Warambo, Paul Kamotho, Patrick Okombo, Suleiman

Milikau, Crispinus Mukhata na Mulama Shitemi. Ahsante kwa ushirikiano wenu ambao umetufikisha mahali tulipo sasa.

Shukrani za dhati kwa shemeji yangu Shem Misian na binti yake Faith kwa msaada mlionipa wakati nilikuwa karibu kukwama. Nawashukuru ndugu zangu David, Zachariah, Samuel, Enock, Nemuel, Daniel na Eric. Pia dada zangu Miriamu, Rebecca, Peris, Florence na Teresa. Siwezi kuwasahau wapwa wangu Nadupoi Nairenke, Ngoitoi, Justus, Joseph, Isaac, Zablon na Geofrey. Asante kwa msaada na ushauri mlionipa ambao uliniongoza kukamilisha safari hii, Mungu awaongoze katika shughuli zenu.

Kwa wale wote walionisaidia kwa njia moja au nyingine na sikuwataja, asante kwa yote mliyonitendea, Mungu azidi kuwaongoza maishani.

# TABARUKU

Kwa marehemu wazazi wangu, Jemimmah Mogesa na Hezron Maobe .

Asante kwa elimu na ushauri mlionipa. Mungu awalaze pema Peponi.

# IKISIRI

Katika utafiti huu wa ukombozi wa mwanamke, tumeona kwamba ukombozi wa mwanamke unamtegemea mwanamke mwenyewe. Mwanamke anafaa kuchukua mstari wa mbele ili kupigania haki zake za kijamii kama njia ya kupinga ugandamizwaji anaotendewa na mwanamume. Ili kutimiza haya inafaa mwanamke ajikomboe katika hali zote za maisha kama vile: kijamii, kiuchumi na kisiasa. Anapofikia hali hii, mwanamke ataweze kujitegemea katika utendakazi na kuchukua uamuzi wa busara katika jamii. Kufanya hivi kutaweza kumwondolea majaribio yanayolenga kumgandamiza.

Katika utafiti huu tumeweza kuonyesha namna wahusika wa kike katika riwaya za Habwe wamejishughulisha na harakati mbalimbali zinazolenga kuwakomboa kutokana na ugandamizaji wa wanaume.

Katika sura ya pili tumeweza kutaja baadhi ya riwaya zingine za mwandishi ambazo kwa ujumla zinanuia kuleta heshima, haki, usawa na ushirikiano katika jimii. Aidha tumeweza kujadili hali mbalimbali za ukombozi wa kijamii, kiuchumi na kisiasa. Tumejadili kuhusu dhuluma wanazopitia wanawake kutoka kwa wanaume. Baadhi ya dhuluma hizi ni: kupewa adhabu kali, kulazimishwa katika ndoa, kubaguliwa katika urithi, kubaguliwa katika taasisi za elimu na kubaguliwa katika uongozi. Ugandamizaji huu hutekelezwa na vyombo vya kijamii kama vile: Utamaduni ndoa na dini.

Katika sura ya tatu na ya nne tumejadili kuhusu harakati za kujikomboa dhidi ya dhuluma za mwanaume. Kupitia riwaya ya *Maumble si Huja.* Tumeonyesha namna mwanamke amejiimarisha kiuchumi na kijamii lakini kwa kiasi kikubwa kwa kutegemea nguvu za

mwanamume. Riwaya hii imeonyesha mwanzo tu wa harakati za ukombozi ambapo mwanamke amejikomboa kwa kiasi kidogo.

Kwa kutumia mali ya mwanamume, mwanamke amejianzishia miradi ambayo imefanikiwa japo kwa kiasi kidogo. Riwaya ya *Fumbo la Maisha,* mwanamke ameweza kujikomboa kiuchumi, kijamii na kisiasa. Amedhihirisha hayo wazi kwa kuanzisha miradi yake ya kiuchumi kama vile biashara, kilimo, na ufugaji. Hatimaye amefikia upeo wa kudai na kupewa haki zake kama vile ardhi haki ya kuiongoza jamii kwa kuchaguliwa mbunge.

## YALIYOMO

UNGAMO ........ ii
SHUKRANI ........ iii
TABARUKU ........ v
IKISIRI ........ vi
YALIYOMO ........ viii
VIFUPISHO ........ xi

**SURA YA KWANZA ........ 1**
1.0 UTANGULIZI ........ 1
1.1 TATIZO LA UTAFITI ........ 3
1.2 MADHUMUNI YA TASNIFU ........ 4
1.3 NADHARIA TETE ........ 5
1.4 SABABU YA KUCHAGUA MADA ........ 5
1.5 UPEO NA MIPAKA ........ 6
1.6 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO ........ 6
1.7 MISINGI YA NADHARIA ........ 10
1.8 NJIA ZA UTAFITI ........ 15
1.9 HITIMISHO ........ 15

**SURA YA PILI ........ 16**
**RIWAYA ZA UTAFITI ........ 16**
2.0 Ukombozi wa Mwanamke katika riwaya za Habwe. ........ 16
2.1 Utangulizi ........ 16
2.2 Maana ya Ukombozi wa Mwanamke. ........ 17
2.3 Dhuluma za mwanamume kwa mwanamke. ........ 18
2.3.1 Adhabu ........ 18
2.3.2 Ndoa za lazima ........ 18
2.3.3 Kufanyizwa kazi ngumu ........ 19
2.3.4 Kubaguliwa katika urithi ........ 19

2.3.5 Kudhulumiwa katika taasisi za elimu ....20
2.4 HARAKATI ZA UKOMBOZI ....21
2.4.2 Harakati za kiuchumi ....22
2.4.3 Harakati za kisiasa ....23
2.5 Riwaya za John Habwe ....23
2.5.1 Muhtasari wa riwaya ya *Maumbile si Huja* ....24
2.5.2 Muhtasari wa riwaya ya *Fumbo la Maisha* ....26
2.6 Hitimisho ....28

**SURA YA TATU ....30**
3.0. Ukombozi wa mwanamke katika riwaya ya Maumbile Si Huja ....30
3.1. Utangulizi ....30
3.2 Ukombozi Wa Mwanamke ....30
3.2.1 Asasi za ndoa ....31
3.2.2 Jukumu la malezi ....34
3.2.4 Biashara ....35
3.2.5 Sheria na haki ....36
3.2.6 Ukuzaji wa vipawa ....37
3.2.7 Ushirikiano ....38
3.3 Hitimisho ....38

**SURA YA NNE ....40**
4.0 Ukombozi wa mwanamke katika riwaya ya *Fumbo la Maisha* ....40
4.1 Utangulizi ....40
4.2 Harakati za ukombozi wa mwanamke ....40
4.2.1 Kuwakabili wanaume wagandamizaji ....40
4.2.2 Kuchukua uamuzi ....42
4.2.3 Mapenzi, umoja na ushirikiano ....44
4.2.4. Kilimo na Ufugaji ....45
4.2.5. Mabadiliko ....46
4.2.6 kampeni dhidi ya ukimwi. ....47

4. 2.7 Kuanzisha vyama vya ushirika. ..........48
4.2.8 Kukuza taaluma zao..........49
4.2.9. Biashara ..........50
4.2.10 Kudai haki..........51
4.2.11 Elimu..........52
4.2.12 Siasa..........54
4.3 Hitimisho ..........56

**SURA YA TANO ..........58**
5.0 Hitimisho ..........58
5.1 Utangulizi ..........58
5.2 Upimaji wa Nadharia..........60
5.3 Mapendekezo..........61

**MAREJELEO ..........62**

## VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| k.h.j | : | Kama hapo juu |
| n.k. | : | nakadhalika |
| T.y | : | Tafsiri yangu |
| Uk. | : | Ukurasa |
| (a) | : | Riwaya ya Maumbile si Huja |
| (b) | : | Riwaya ya Fumbo la Maisha |

## SURA YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

Utafiti huu utashughulikia ukombozi wa mwanamke katika riwaya za Habwe: *Maumbile si Huja* (1995) na *Fumbo la Maisha* (2008). Utanzu wa riwaya na hasa kabla ya miaka ya 1990 ulielekea kuzingatia maudhui ya mapenzi, ndoa, maadili, ukoloni na utendakazi. Mfano wa riwaya hizi ni kama: *Utubora Mkulima* (1968) na *Siku ya Watenzi Wote* (1968) za Shaaban Robert, *Usilie Mpenzi Wangu* (1971) ya Ngugi wa Thiong'o na *Kaburi bila Msalaba* (1969) ya Kareithi.

Riwaya zinazohusu ukombozi wa mwanamke zilianza kushika kasi miaka ya1990, riwaya hizi zilihusu dhuluma anazotendewa mwanamke na mwanamume ambazo zinachochewa na asasi za kijamii kama utamaduni (Ndoa, dini,taasisi za elimu na imani na itikadi za kijamii). Riwaya hizi zilizingatia zaidi suala la dhuluma anazotendewa mwanamke na mwanamume.

Walibora (1996) katika riwaya yake ya *Siku Njema* ameonyesha namna suala la malezi ya watoto linavyoachiwa mwanamke na mwanaume ambaye anakosa kuwajibikia jukumu lake la uzazi. Hii ni aina ya dhuluma anazotendewa mwanamke.

Wamitila (1999) katika *Nguvu ya Sala,* anaonyesha jinsi dini inavyomdhulumu mwanamke. Kwa kuegemea tafsiri potovu za biblia, Ngunzi anamlazimisha mkewe na wasichana wake kufuata matakwa yake bila upinzani wowote. Hii ni dhuluma nyingine anazotendewa mwanamke.

Mbatiah (2005) katika riwaya ya *Upotevu* anaonyesha namna mwanamke anavyogandamizwa na jamii. Mwandishi huyu anaonyesha namna mwanamke anavyolazimishwa na asasi za kijamii, kujiingiza katika maovu ili kujikimu kimaisha. Mwanamke analazimika kujiingiza katika

ukahaba kama njia moja ya kujikimu kimaisha. Hii ni aina nyingine ya dhuluma ambayo mwanamke anatendewa na jamii.

Katika riwaya ya *Msimu wa Vipeopeo* (2006), Wamitila anamsawiri mwanamke katika mazingira hasi ya ndoa. Mwandishi huyu anaonyesha jinsi mwanamke anavyodhulumiwa na mwanamume katika maisha ya ndoa.Ameonyesha jinsi wahusika wa kike Melissa na Miranda wanavyojitetea dhiti ya dhuluma hizi.

Suala la mwanamke na hasa dhuluma anazotendewa na mwanamume limezindi kuwashughulisha watafiti wengi. Baadhi yao ni kama Rutele(1990). Mtafiti huyu amechunguza namna nguvu za ubabedume katika riwaya za Ngugi wa Thiong'o zinavyochangia katika kumgandamiza mwanamke. Ubabedumu ni sababu nyingine inayochangia kumdhulumu mwanamke katika jamii.

Mugambi (1983) ameangazia kilio cha wanyonge, katika riwaya za Said Mohamed na kuonyesha jinsi mwanamke anavyodhulumiwa na mwanamume. Aidha Okemwa (2008) amewachunguza waandishi wa Kenya ambao wameandika juu ya mwanamke, suala ambalo Dorithy (2007) ameliangazia katika nchi jirani ya Tanzania. Mwandishi huyu ameuangazia ubabedume na suala la utabaka katika riwaya za kezilahabi. Amejaribu kuonyesha namna mwanamke anavoyodhulumiwa katika mazingira haya. Ingawa riwaya hizi zimeangazia mazingira ya nchi ya Tanzania masuala ya ukombozi wa mwanamke yanaelekea kushabihiana katika nchi nyingi na hasa za eneo la Afrika Mashariki

.

Kwa kuangazia kazi hizi za fasihi tunanuia kudhibitisha kwamba, ingawa suala la mwanamke limeangaziwa kwa mapana, nyingi za kazi hizi zimeangazia suala la kugandamizwa kwa mwanamke, hatuna ushahidi wa kazi yoyote ya kifasihi ambayo imeangazia mikakati anayotekeleza mwanamke ili kujinusuru kutokana na ugandamizaji huu. Kwa sababu hii utafiti huu unanuia kuchunguza ukombozi wa mwanamke katika riwaya za Habwe: *Maumbile si Huja* (1995) na *Fumbo la Maisha* (2008) kwa madhumuni ya kubainisha harakati za ukombozi wa mwanamke. Aidha tunatarajia kudhibitisha kwamba mwanamke amefaulu kujikomboa katika riwaya ya *Fumbo la maisha.*

Suala la ukombozi wa mwanamke ni mojawapo ya masuala ibuka katika fasihi ya Kiswahili ambalo lina asili yake katika mataifa ya magharibi. Suala hili linaendelea kukita mizizi yake katika taifa la Kenya. Sababu hii inatuongezea ari ya kutaka kutoa mchango wetu wa kiusomi. katika uwanja huu wa fasihi.

## 1.1 TATIZO LA UTAFITI

Suala la ukombozi wa mwanamke dhidi ya ugandamizaji wa mwanamume limeshughulikiwa na watafiti wengi. Watafiti hawa wameangazia jinsi mwanamke anavyogandamizwa na mwanamume kupitia vyombo vya utamaduni kama vile: Asasi za ndoa, taasisi za elimu, dini,itikadi na mila za jamii. Baadhi ya watafiti ambao wameshughulikia suala hili ni Ndungo(1985). Mwandishi huyu ametafiti mabadiliko ya kihistoria ya mwanamke katika fasihi ya Kiswahili. Ameonyesha jinsi mwanamke alivyogandamizwa katika nyakati mbalimbali za kihistoria kama vile: Kabla ya uhuru, wakati wa kupigania uhuru na kipindi cha baada ya uhuru.

Katika vipindi hivi vyote mwanamke anatazamwa kama kijakazi jambo ambalo linazidisha dhuluma dhidi yake.

Mugambi (1983) amezihakiki riwaya tatu za Said Mohamed kwa kuangazia aina za ugandamizaji ambao unaelekezwa kwa wanyonge. Mfano wa wanyonge hawa ni wanawake na watoto ambao wanagandamizwa na wenye nguvu ambao ni wanaume.

Ingawa watafiti hawa miongoni mwa wengine wametoa mchango mkubwa kwa kuonyesha jinsi mwanamke anavyogandamizwa na mwanamume, tafiti zao hazijaonyesha jinsi mwanamke atakavyojinusuru kutokana na ugandamizaji huu. Utafiti wetu utaangazia harakati anazofanya mwanamke ili kujikomboa kutokana na ugandamizaji wa mwanamume. Aidha tunakusudia kudhibitisha kwamba mwanamke hatimaye amefaulu kujikomboa katika riwaya ya *Fumbo la Maisha.*

## 1.2 MADHUMUNI YA TASNIFU

Tasnifu hii ina madhumuni yafuatayo:

i) Kuchunguza jinsi mwandishi anavyoshughulikia harakati za mwanamke za kujikomboa kutokana na dhuluma za mwanamume.

ii) Kutathmini changamoto zinazomkwamisha mwanamke katika juhudi zake za kujikomboa kutokana na dhuluma za mwanamume

iii) Kuthibitisha kwamba mwanamke amefaulu kujikomboa katika riwaya *Fumbo la Maisha.*

iv) Kujaribia ufaafu wa nadharia ya ufeministi wa kirasimi katika kuzihakiki riwaya za Habwe.

## 1.3 NADHARIA TETE

Katika utafiti huu tutaongozwa na nadharia tete zifuatazo:

i) Ukombozi wa mwanamke unamtegemea mwanamke mwenyewe.

*ii)* Mwanamke amefanikiwa kujikomboa kutokana na dhuluma za mwanamume katika riwaya ya Fumbo la Maisha.

*iii)* Utamaduni ndio kikwazo kikubwa kinachokwamiza juhudi za mwanamke za kujikomboa kutokana na dhuluma za mwanamume.

*iv)* Nadharia ya Ufeministi wa Kirasimi inajitosheleza katika kuhakiki riwaya ya *Maumbile si Huja* na *Fumbo la Maisha.*

## 1.4 SABABU YA KUCHAGUA MADA

Suala la ukombozi wa mwanamke limeshika kasi nchini Kenya miaka ya 1990, tafiti nyingi zilizotangulia zinaonyesha kuegemea zaidi kwenye aina za dhuluma anazotendewa mwanamke na mwanamume kama tulivyodhibitisha katika utangulizi wetu. Sababu zetu za kuchagua mada hii ni kuangazia harakati mbalimbali zinazofanywa na mwanamke katika juhudi zake za kujikomboa kutokana na ugandamizaji wa mwanamume. Eneo hili la utafiti linaonekana kutoshugulikiwa na watafiti wanaochunguza suala la ukombozi wa mwanamke.

Aidha tafiti nyingi zinaonyesha kwamba mwanamke anazidi kudhulumiwa na mwanamume na hajafanikiwa kujikomboa kutokana na dhuluma hizi. Katika kazi hii tunadhamiria kuonyesha kwamba mwanamke amefanikiwa kujikomboa katika riwaya ya *Fumbo la Maisha.*

Tumechagua kutafiti ukombozi wa mwanamke katika riwaya mbili za Habwe: Kwanza, kuonyesha dhuluma ambazo mwanamke amekumbana nazo katika jamii na jitihada zake za kujikomboa katika riwaya ya *Maumbile si Huja.* pili, kuonyesha namna juhudi zake za kujikomboa zinavyofanikiwa katika jamii na upeo wa ukombozi wake katika riwaya ya *Fumbo la Maisha.*

### 1.5 UPEO NA MIPAKA

Utafiti huu ni wa kifasihi. Nia yetu ni kuangazia ukombozi wa mwanamke kutokana na ugandamizaji wa mwanamume.

Tutajikita katika riwaya mbili za Habwe: *Fumbo la Maisha(2008)* na *Maumbile si Huja(1995).* Tutataongozwa na nadharia ya ufeministi wa kirasimi katika uhakiki wetu.Aidha tutashugulikia maudhui ya ukombozi wa mwanamke katika riwaya hizi mbili.

### 1.6 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO

Suala la mwanamke limeshughulikiwa kwa upana katika fasihi ya Kiswahili. Waandishi wengi waliolishughulikia suala la mwanamke wametoa mitazamo mbalimbali kuhusu mwanamke katika jamii. Baadhi ya waandishi hawa ni Ndungo (1985). Mwandishi huyu ameangazia mabadiliko ya kihistoria kuhusu maisha ya mwanamke katika fasihi ya Kiswahili. Akirejelea kazi tatu za kifasihi, *Utendi wa Mwanakupona, Kaburi bila Msalaba* na *Utengano,* Ndungo anaonyesha namna mwanamke anavyodhulumiwa katika jamii.Baadhi ya dhuluma hizi ni za

kisiasa, kijamii na kiuchumi.Mwandishi huyu ameshindwa kuonyesha namna mwanamke anaweza kujinasua kutokana na dhuluma hizi.

Majumdar (1953) anasema kuwa ingawa mwanamke na mwanamume wana uwezo sawa kielimu, mara nyingi jamii hupenda kumdunisha mwanamke kwa kumtazama kama jinsia dhaifu na hivyo kumnyang'anya haki zake za kikazi kwa kumpa malipo ya chini akilinganishwa na mwanamume. Mawazo haya yanaungwa mkono na Brown (2007:57) anaposema,

> ingawa mwanamke ana haki sawa na mwanamme kisheria, tofauti hujitokeza pale wanapopewa kazi za mapato ya viwango tofauti. Kwa sababu ya kazi za kiwango duni wanaopewa wanawake, wanawake wengi, hupata pato la chini sana wakiwalinganishwa na wanamume. Huu ni ugandamizi unaolenga kumdunisha mwanamke. Katika hali hii mwanamume humtazama mwanamke kama kiumbe duni ambaye hafai kuwa na haki sawa naye (T.Y).

Chacha (1986) ametafiti riwaya ya *Rosa Mistika* na kuonyesha jinsi mazingira mbalimbali yanavyotumiwa na mwandishi kuwadhulumu wahusika wa kike akiwemo Rosa Mistika. Kazi hii ni muhimu kwa utafiti wetu kwa sababu inatupa taswira ya masaibu yanayomkumba mwanamke katika maeneo mengine ya Afrika Mashariki.

Lugano (1989) aliangazia nafasi ya mwanamke katika riwaya nne za Kezilahabi ambazo ni: *Rosa Mistika, Kichwamaji, Dunia Uwanja wa Funjo* na *Gamba la Nyoka.* Mwandishi huyu

ameonyesha namna waandishi wamemsawiri mwanamke katika jamii ya Tanzania. Katika kazi hizi, mwanamke anatazamwa kama kiumbe duni.

Mugambi (1983) ameangazia kilio cha wanyonge katika riwaya za Said Mohamed na kubainisha aina tatu za ugandamizaji ambazo ni: Ugandamizwaji wa wanyonge, ugandamizwaji wa wenye nguvu na ugandamizwaji wa kimazingira. Katika kazi yake Mugambi anavilenga vizazi vyote vinavyogandamizwa kama vile; wanawake, watoto na maskini. Kazi yake kwa ujumla inaangazia swala la ugandamizwaji kwa upana zaidi tofauti na kazi yetu ambayo inaangazia ukombozi wa mwanamke.

Mbatiah (1997) anadai kuwa, mila na desturi za waswahili zimechangia sana kumdunisha mwanamke katika jamii zao. Anaeleza kuwa baadhi ya desturi hizi ni zile zinazohusu ndoa, dini na utamaduni. Hivi ni vyombo vikubwa vya ugandamizaji. Hata hivyo Mbatia hajatoa suluhu kuhusu namna mwanamke anavyoweza kujikomboa kutokana na ugandamizaji huu.

Dorithy (2007) ameuangalia ubabedume na utabaka katika riwaya mbili ya Kezilahabi, *Rosa Mistika* na *Kichwamaji.* Katika kazi yake ameonyesha jinsi mwanamume anamgandamiza mwanamke. Aidha ameonyesha namna asasi za ndoa, dini na utamaduni zinavyochangia katika kumgandamiza mwanamke katika jamii. Utafiti wetu unanuia kuangazia dhuluma anazozipata mwanamke na namna anavyoweza kujikomboa kutokana na dhuluma hizi.

Stanford (1998) Ameandika kuhusu mwanamke katika nchi ya Afrika Kusini. Ameonyesha jinsi anavyodhulumiwa na utawala unaozingatia ubaguzi wa rangi. Mwandishi huyu

ameangazia namna wanafunzi wa kike wanavyotayarishwa katika taasisi za elimu kuwa wafanyikazi wema wa wanaume.Aidha mwandishi huyu anaeleza kuwa mfumo wa elimu ambao ulitumiwa katika nchi hii uliendeleza ugandamizaji wa wanawake. Akimunukuu Hughes (1990:216) Stanford anasema kuwa, mfumo wa elimu uliotumika vyuoni ulihimiza kusoma na kukariri Bibilia, kuandika,hesabu, jeografia pamoja na kufanya kazi ya mikono kama ushonaji nguo, kulima, ufugaji wa kuku, upishi na usafi wa nyumbani. Mafunzo haya yote yalidhamiria kuendeleza udhalimu wa wanaume kwa wanawake.Wanawake walihimizwa kuwa safi na kujifunza kuwatumikia mabwana zao. Aidha kazi kubwa ya mwanamke ilikuwa ni upishi na kuzingatia usafi katika familia na kwa hivyo jamii ilihimiza wanawake wapewe mafunzo ya hali ya juu kuhusu kazi za nyumbani. Dhamira kuu ya kufanya hivyo ilichochewa na mpango wa wanaume wa kuwatayarisha wanawake ili kuendelea kuwafaa katika maisha yao ya ugandamizaji.

Okemwa (2008) Amewatazama waandishi wa Kenya kama: Grace Ogot, Ngugi Wa Thiongo na Sammy Kahiga. Mwandishi huyu anaonyesha maendeleo ambayo mwanamke amepata tangu miaka ya 1960, 1970 na 1980. Aidha, ameangazia mabadiliko yaliyopatikana katika sekta ya elimu, uchumi, siasa na jamii. Utafiti huu unatupa mwangaza wa mitazamo mbalimbali ya waandishi wa awali wa hapa nchini walioandika kuhusu ukombozi wa mwanamke.Kwa kuangazia waandishi hawa tunanuia kudhibitisha kwamba ingawa suala la ukombozi wa mwanamke limeangaziwa kwa kina,waandishi hawa wameshindwa kuonyesha namna mwanamke anavyopaswa kufanya ili kujikomboa kutokana na dhuluma za mwanamume.

Kwa kujikita katika riwaya za Habwe *Maumbile si Huja* na *Fumbo la Maisha*, tunatarajia kuonyesha mikakati mbalimbali ambayo mwanamke amechukua ili kujikomboa kutokana na ugandamizi huu. Aidha tutathibitisha kwamba mwanamke hatimaye amefaulu kujikomboa katika riwaya *Fumbo la Maisha.*

## 1.7 MISINGI YA NADHARIA

Utafiti huu unaongozwa na nadharia ya Ufeminist wa kirasimi.

Watson, J. na Hill (2000 :112) anasema kuwa ufeministi ni dhana yenye migao mingi ambayo inahusiana na maendeleo na udumishaji wa haki sawa za kijamii na kisiasa kwa wanawake. Nadharia hii hupinga tofauti za kijinsia pamoja na chukulizi za kitamaduni zinazoukweza ubabedume unaowagandamiza wanawake.

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu(2006)* wanaeleza ufeministi kama, tapo la kupigania ukombozi, haki na usawa wa wanawake.Wazo hili linaungwa mkono na Mbatiah (2001:87) ambaye anaeleza ufeministi kuwa nadharia ya fasihi ambayo inajishughulisha na utetezi wa wanawake dhidi ya ugandamizwaji katika jamii yenye mifumo iliyodhibitiwa na wanaume.

Wamitila (2002:157) anaelezea, ufeministi kuwa msingi, msukumo na nia ya kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kiutamaduni, kidini, kisiasa na kiuchumi.Ufemiisti hudadisi misimamo na itikadi za kiume, huangazia misimamo tawala na kuzishambulia dhana za kiume kama ubabedume.

Kwa maoni ya wataalam hawa, ufeministi ni nadharia inayopigania ukombozi wa mwanamke kwa kushambulia asasi za kijamii, kidini, kisiasa na kiutamaduni ambazo huchangia katika kumgandamiza mwanamke.

Wafula na Njogu(2007:21) wanaeleza Urasimi kama, wakati maalum ambapo misingi ya kazi za sanaa huwekwa na kukubalika kuwa vipimo bora kwa kazi nyingine. Kwa kuoanisha dhana hizi mbili, tunapata Ufeministi wa kirasimi kama kipindi maalum ambapo sanaa ya kifasihi inayozungumzia ukombozi , haki na usawa wa mwanamke inachukuliwa kama kipimo bora cha kazi nyingine zinazohusu ukombozi wa mwanamke. Nadharia ya Ufeministi wa Kirasimi ilijifunga katika mawazo ya kwanza ya ufeministi ambayo yalipinga dhuluma zote za mwanamume kwa mwanamke.

**Asili ya nadharia ya ufeministi wa Kirasmi**

Watson, J. na Hill (2000:45) wanasema kuwa urasimi ulizinduliwa na mwanafilosofia wa Kijerumani Karl Marx (1818-83). Kwake urasimi ulikuwa na mahusiano katika uzalizaji mali. Marx anaeleza kuwa vipindi vya nyakati tofauti hutawaliwa na matabaka mawili ambayo ni ya wenye nguvu na maskini.Wenye nguvu na maskini wote walihusika katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kisiasa katika nchi. Kulingana na Marx tabaka la wenye nguvu hutawala matabaka mengine kitamaduni, kimawazo na kisiasa.

Dhana ya urasimi ya Karl Marx ilitoa mawazo ya kimsingi ya nadharia ya Ufeministi wa Kirasimi. Mawazo haya yaliwachochea wanafilosofia ambao walipinga mila na tamaduni zote zinazomgandamiza mwanamke na kumpendelea mwanamume .Wanafilosofia hawa walihimiza

wanawake kutendewa haki *jinsi ilivyo kwa wanaume. Mawazo haya ya ufeministi yaliendelezwa* na Mary Wollstonecraft(1872) katika kazi yake ya *Avindication Of the Rights of Women.*Wollstonecraft akishirikiana na John Stuart Mill walikubaliana kuwa tofauti kubwa ya kijinsia ya mwanamke na mwanamume husababishwa na hali ya mazingira kuliko matukio ya kiasili. Waliafikiana kuwa mtazamo wa mwanamume kumuona mwanamke kama kijakazi ni njia moja ya kumgandamiza. Walihimiza haki na na usawa kwa wanawake katika jamii. *Avindication Of the Rights of Women* ya Mary Wollstonecraft ndio ilikuwa chapisho la kwanza la kike nchini Uingereza.

Waandishi wengine ambao waliyaunga maoni ya Wollstonecraft ni Godwin ambaye alikuja kumuoa baadaye. Mawazo ya Wollstonecraft yalisaidia kuleta haki na usawa wa kijinsia ambao ulinuia kuboresha maisha ya mwanamke nchini Uingereza na Marekani.

Nadharia ya ufeministi iliendelezwa na wanaharakati wengine kama Sojourner Truth (1851). Katika chapisho lake *The Changing Woman,* Sojourner alielezea vile wanawake wote walikuwa sawa katika utendakazi na hivyo kupinga misingi yote ya kuwangalia wanawake kwa kuzungatia rangi na jinsia. Alieleza kuwa dhuluma zote anazopata mwanamke husababishwa na uchukulio hasi alionao mwanamume kwa mwanamke ambao unamdunisha.Anasisitiza kwamba wanawake wapewa haki zao bila kujali hali zao za kijinsia. Mawazo ya sojourner yanaungwa mkono na Susan B. Anthony (1872) ambaye anasisitiza kwamba sheria hazikuundiwa mwanamke pekee.Anadai kwamba, ikiwa sheria hizo hazimsaidii kujihami basi hazina maana kwake.

Wanaharakati wengine waliochochewa na mawazo ya Wollstonecraft walikuwa Beauvoir (1949). Katika kazi yake *The Second Sex,* anazishambulia baadhi ya asasi za jamii ambazo zinachangia katika ugandamizaji wa mwanamke ambazo ni ndoa, utamaduni na dini. Anapinga mtazamo hasi kwa wanawake na kupendekeza mwanamke kutazamwa kama kiumbe sawa na mwanamume. Anasisitiza kuwepo kwa usawa wa kijinsia kama njia ya kumkomboa mwanamke kutoka kwa ugandamizwaji unaotekelezwa na jamii. Wanawake kama wanadamu wengine wanahitaji usawa na udumishwaji wa haki zao.

Katika jamii nyingi wanawake wamekua kama wafamaji ambao hawana pa kushika, De Beauvoir (1949:16) anasema kwamba mazingira na tamaduni anazokulia mwanamke huchangia katika ugandamizaji huu na hivyo kumfanya kukubali kuwa kiumbe dhaifu. Hali hii inamfanya kama chombo cha jamii cha kuendeleza utamaduni huu dhalimu. De Beauvoir(k.j.h) anamtazama mwanamke kama mtu ambaye mawazo yake yametekwa bakunja na mwanamume kwa kusema kuwa, mwanamume anaweza kufikiri na kuamua bila mwanamke lakini mwanamke hawezi kufikiria na kuamua bila usaidisi wa mwanamume. Yeye hufanya kile mwanamume anachomwamuru kufanya, mwanamke anatazamwa kama kiumbe wa starehe.

Mawazo kama haya hutilia mbolea na kuchochea kudhulumiwa kwa mwanamke katika jamii. De-Beauvoir(k.h.j) analeza kuwa ndoa ni mojawapo ya asasi za kitamaduni ambazo zinampa mwanamume uwezo mkubwa wa kumtazama mwanamke kama chombo cha anasa na starehe. Dini inachangia katika kuhalalisha mtazamo huu hasi wa mwanamume kumhusu mwanamke.

Moi (1985) Katika kazi yake *Sexual / Textual Politics* anaunga mkono kuwepo kwa nadharia ambayo inaondoa mipaka yote inayotenganisha mwanamke na mwanamume kwa misingi ya kijinsia. Anapendekeza kutumiwa kwa nguvu ili kuweza kukabiliana na aina zote za udhalimu, waliowekewa ili kuwatenganisha na wanaume na hivyo kuwanyima haki na usawa wa kijinsia. Moi, akimnukuu Kate Millet katika kazi yake, *The Essence of Politics* anaelezea hali inayomkabili mwanamke kama vile, upinzani wa wanaume unaolenga kusambaratisha harakati za mwanamke za kujikomboa. Akimnukuu Mary Ellmann, katika kazi yake *Thinking About Women.* Moi anaonyesha jinsi mwanamke anavyosawiriwa katika kazi zilizoandikwa na wanaume. Kazi hizi zina mapendeleo fulani ya kijinsia. Anajaribu kuonyesha kwamba ni muhimu kwa wanawake kuchukua mstari wa mbele katika kujikomboa.

Eagleton (1991:7) Katika kazi yake ya *Feminist Literary Crticism* anaunga mkono mawazo ya Woolf, Moi, na Showalter, kwa kusema kwamba, kile ambacho kinamfanya mwanamke kuonekana tofauti katika jamii ni, kukosa uungwaji mkono wa kijinsia na jamii, ukosefu wa elimu ya kutosha, ukosefu wa mali, uoga na haya.

Kwa ujumla ufeministi hupinga aina zote za ugandamizaji anaotendewa mwanamke katika jamii. Hupinga ndoa za lazima, kubaguliwa katika urithi na uongozi. Tumechagua kulitafiti suala la ukombozi wa mwanamke kwa kuzingatia nadharia ya ufeministi wa kirasimi. Sababu ambazo zimetushawishi kuichagua nadharia hii ni kwamba, nadharia hii inaafiki mada yetu ya ukombozi wa mwanamke. Kwa kuwa ufeministi wa kirasimi huangazia masuala ya wakati maalum ambapo misingi ya kazi za kifasihi huwekewa vipimo vya kuwa kazi bora, tunanuia

kuonyesha kwamba riwaya ya *Fumbo la Maisha* inaafiki kuwekewa msingi wa kuitwa riwaya bora ya ukombozi wa mwanamke.

## 1.8 NJIA ZA UTAFITI

Utafiti huu ni wa maktabani. Tutasoma kazi ambazo zimeshughulikia ukombozi wa mwanamke. Aidha tutazisoma riwaya zingine za Habwe ili kupambanukiwa na falsafa inayomwongoza katika uandishi wake. Tutamhoji mwandishi mwenyewe ili kupata maoni zaidi kuhusu kazi zake.

## 1.9 HITIMISHO

Katika sura hii ya kwanza tumeangazia masuala ya kimsingi yanayohusiana na utafiti huu.Masuala haya ni pamoja na: Utangulizi, tatizo la utafiti, na madhumuni ya utafiti huu na sababu ya kuchagua mada. Aidha tumeshughulikia nadharia tete, yaliyoandikwa kuhusu somo, njia za utafiti. Hatimaye tumeangazia upeo na mipaka. Madhumuni ya sehemu hii ni kuweka msingi wa utafiti wetu wa ukombozi wa mwanamke.

Katika sura ya pili tutachunguza ukombozi wa mwanamke katika riwaya za Habwe. Aidha tutafafanua maana ya ukombozi na dhuluma zinazomkabili mwanamke katika riwaya za Habwe.

# SURA YA PILI

# RIWAYA ZA UTAFITI

## 2.0 Ukombozi wa Mwanamke katika riwaya za Habwe.

### 2.1 Utangulizi

Katika sura ya kwanza, tumechunguza masuala ya kimsingi yanayohusiana na utafiti huu,ambayo ni: Utangulizi wa mada, tatizo la utafiti, madumuni ya utafiti, nadharia tete na upeo na mipaka. Aidha tumechunguza kuhusu yaliyoandikwa kuhusu somo, msingi wa nadharia, njia za utafiti na kuhitimisha.

Katika sura hii ya pili tutachunguza ukombozi wa mwanamke katika riwaya mbili za Habwe:*Maumbile si Huja* (1995a) na *Fumbo la Maisha* (2008b). Aidha tutachunguza maana ya ukombozi wa mwanamke kama njia ya kuweka msingi wa uhukiki huu. Halafu tutachunguza dhuluma zinazowakabili wanawake kama njia ya kuweka msingi imara wa uhakiki wa mada yetu ya 'ukombozi wa mwanamke.'

Kwa kuangazia dhuluma za mwanamke tutapata kigezo mwafaka cha kutumia katika kuhakiki ukombozi wa mwanamke. Baadhi ya dhuluma tutakazozichunguza ni: Kupewa adhabu kali na mwanamume, kubaguliwa katika taasisi za elimu, kushirikishwa katika ndoa za lazima, kubaguliwa katika uongozi na kuachiwa majukumu ya malezi. Aidha, tutachunguza dhuluma za kubaguliwa katika urithi, na dhuluma za kimapenzi. Halafu tutajadili harakati mbalimbali za ukombozi wa mwanamke kama vile: Za kijamii,kiuchumi na kisiasa na kueleza jinsi ambavyo zimeathiri ukombozi wa

mwanamke. Tutaguzia riwaya zingine za Habwe na hatimaye tutatoa muhtasari wa riwaya ya *Maumbile si Huja* na *Fumbo la Maisha*

## 2.2 Maana ya Ukombozi wa Mwanamke.

Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004:431) wanaeleza ukombozi kama 'uokoaji wa watu kutoka kwenye hali mbaya ya udhalimu au hali duni'. Kwa hivyo ukombozi wa mwanamke unahusu harakati za mwanamke kujiokoa kutoka kwenye hali mbaya ya udhalimu wa mwanamume. Ukombozi wa mwanamke unalenga kutetea udumishaji wa haki na usawa wa mwanamke katika jamii. Ukombozi wa mwanamke unaweza tu kupatikana kupitia kupinga hali zote za maisha zinazomnyima mwanamke haki sawa na mwanamume.

Ukombozi wa mwanamke unahusu juhudi za mwanamke kupinga dhuluma anazotendewa na mwanaume. Dhuluma hizi humnyima haki zake za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Wanawake wanaweza kujikomboa kwa njia mbalimbali kama: Kuwania viti vya uongozi, kuwa huru kutumia vyombo vya mawasiliano, kupewa uhuru wa kufanya biashara na ajira yenye malipo sawa na mwanamume. Aidha mwanamke anapaswa kulindwa kwa mujibu wa kisheria kutokana na dhuluma za mwanamume na anapasa kupewa haki zake za kielimu. Mwanamke anaweza kuanzisha miradi ya kiuchumi kama vile,ufugaji wa kuku, ufumaji na uchoraji kama njia ya kujikomboa (Porter 2002).

### 2.3 Dhuluma za mwanamume kwa mwanamke.

#### 2.3.1 Adhabu

Mwanamke hudhurumiwa kwa kupewa adhabu kali wakati makosa yanapotokea ambayo yanapaswa kusuluhishwa kwa njia ya amani. Adhabu anayopewa ni kama vile kupigwa, kutukanwa na kutalikiwa ambazo hazisuluhisha matatizo yoyote ila kuendeleza ugandamizi. Kwa sababu ya adhabu hizi wanawake wengi wamepoteza maisha yao na wengine kutengana na familia zao. Mfano wa matusi na adhabu hizi:

> "Huyu mwanamke ni mjeuri sana.Sitaki mwanamke mwenye ubongo kama uporo.Wanawake wa enzi hizi wamejaa maringo. Ndiyo, wamejaa uchimbi na siutaki kabisa" (uk.19a).
>
> Mgeni na Said waliposikia kisa hicho walijongea karibu ili waandamane na hao wafanyibiashara. Mfanyibiashara akaendelea kueleza kuwa eti mke huyo alipigwa na mmewe karibu afe (uk.48a).

#### 2.3.2 Ndoa za lazima

Suala la ndoa ni mojawapo ya masuala yanayohusu haki ya mwanamke. Kumchagua mpenzi wa kuoa ni haki ya mwanamke. Suala la wazazi kuwachagulia watoto wao wachumba ni kuwanyima haki zao za kimsingi za kujiamulia maisha yao. Ndoa za aina hizi mara nyingi haziduma kwani hukumbwa na matatizo ya kutoelewana.Ushahidi wa madai haya unaonekana katika mjadala kati ya Omar na Suleiman ambao wanaeleza kwamba ndoa kati ya Amina na Juma ilipangwa na babake Amina kwa kuzingatia kigezo cha mali. Ndoa hii ilikumbwa na matatizo mengi na mwishowe ikasambaratika (uk.80a).

Sauda analalamika kuwa kuja kwake mjini kunasababishwa na babake kumlazimisha kuolewa.Anaeleza:

> “Baba na mama walitaka kuniuza kama kitatange sokoni.Mzee Ramadhan alikuja nyumbani akitaka mke wa tatu.Kwa kuwa alitaka kuwapa mali,mama na baba walinishurutisha niwe mkewe” (uk.40a).

### 2.3.3 Kufanyizwa kazi ngumu

Kwa miaka mingi majukukumu ya malezi ya watoto, kazi za nyumbani kama kuosha vyombo, kupika, kufua nguo na kubeba mizigo ya shambani ni majukumu ambayo yameachiwa wanawake. Suala hili limechukuliwa na wanaume kama kazi rahisi isiyostahili nguvu. Katika riwaya ya *Fumbo la Maisha* (uk.22b ), mwandishi anasema, Konya alikuwa mume wa kuzaa lakini hakuwa mume wa kulea. Mwanamke ameachiwa mzigo mkubwa wa kulea watoto na kugharamia mahitaji ya familia ya kila siku ilhali mwanamume anaachwa kulewa na kungoja kulishwa na mwanamke. Hii ni dhuluma kwa wanawake.

### 2.3.4 Kubaguliwa katika urithi

Katika jamii nyingi za kiafrika na hususan nchini Kenya suala la urithi linamtabua mwanamume kama mrithi. Mwanamke huchukuliwa kama bidhaa ya kurithiwa lakini si kiumbe wa kurithi. Mali ya mzazi ni haki kwa watoto wake wote bila kujali jinsia. Mwanamke Kutohusishwa katika urithi ni njia ya kuwagandamiza.

Katika riwaya ya *Fumbo la Maisha,* Mwanaisha anabaguliwa katika urithi wa mali ya baba yake Jambo hili la kutowarithisha wanawake, halikuanzia kwa Mwanaisha bali hata mamaye mzazi ananyimwa haki ya kumrithi mumewe na watoto wake aliowazaa(uk.188).

**2.3.5 Kudhulumiwa katika taasisi za elimu**

Mwanamke anadhulumiwa katika tasisi za elimu kwa njia mbalimbali. Mwanaisha anapachikwa mimba na mwalimu wake akiwa bado mchanga. Konya ambaye anaelewa taaluma ya ualimu inavyosema, anawachiliwa huru bila kulazimishwa kuwajibikia kitendo chake. Isitoshe mfumo wa sheria zinazotumika shuleni unaelekea kumpendelea mwanamume na kumgandamiza mwanamke. Mwananaisha anafukuzwa shuleni kwa kuwa mjamzito, anapofika nyumbani akitarajia usaidizi wa wazazi wake, baba mzazi anamfukuza kwa mikuki, mishale, ngao na mbwa kama jambazi sugu. Ushahidi huu unaonyesha dhahiri namna mwanamke anavyodhulumiwa na taasisi za elimu na jamii kwa ujumla (*Fumbo la Maisha* k.h.j:1)

Pili, wazazi huwaachisha wasichana shule na kuwalazimisha waolewe ili wapate mali ya kuwalipia watoto wavulana karo. Ushahidi huu unajitokeza katika riwaya ya *Maumbile si Huja(k.h.j:40)*. Sauda anaeleza kuwa wazazi wake walimlazimisha aolewe kwa mzee Ramadhan ili waweze kupata mali ya kuwalipia karo ndugu zake wa kiume.Hii ni dhuluma kubwa kwa mwanamke.

Elimu ni msingi wa maisha kwa jinsia zote ambao ni muhimu kwa kila mmoja. Inafaa wanawake waelimishwe ili waweze kupata mwongozo bora wa maisha. Mtazamo hasi wa kumbagua mwanamke katika elimu ni njia moja ya kuendeleza dhuluma dhidi yake.

### 2.3.6 Kubaguliwa katika uongozi

Mwanamke amebaguliwa katika uongozi. Mwanamke anatazamwa kama kiumbe duni katika jamii ambaye hawezi kuwaongoza watu. Mwanaisha anapotangaza msimamo wake wa kuwania kiti cha Ubunge cha Telek, baadhi ya watu wanasema. "Binti atagombaniaje ubunge kwao? Ikiwa ameshindwa kuolewa, ubunge ndio ataweza''(uk.191).

Kudhulumiwa kwa mwanamke kunachangiwa pakubwa na taasubi za kiume ambazo humzuia kupata haki zake za uongozi. Nyadhifa kubwa katika uongozi wa nchi zimetengewa wanaume. Hii ni njia moja ya kuendeleza dhuluma kwa mwanamke.

## 2.4 HARAKATI ZA UKOMBOZI

Harakati za ukombozi wa mwanamke zinahusu shughuli za mwanamke kupigania haki zake. Baadhi ya haki za mwanamke ni kupewa nafasi sawa za uongozi, umiliki wa mali na kukomeshwa kwa aina yoyote ya ugandamizaji. Harakati za ukombozi wa mwanamke zinalenga kumpa mwanamke nguvu za kujitegemea kijamii,kiuchumi na kisiasa.Ingawa harakati hizi zina mahusiano makubwa tutazishughulikia kibinafsi.

### 2.4.1 Harakati za kijamii

Harakati za kujikomboa kwa mwanamke kijamii, zinahusu kuwapa uhuru wa kutoa maamuzi kuhusu maswala ya kijamii kama vile ndoa, utamaduni na dini. Mwanamke aliyejikomboa kijamii hujiamlia mchumba wa kumwoa, hurithishwa mali ya jamii na kupewa nafasi za kielimu sawa na mwanamume.

Harakati za kujikomboa kwa mwanamke zimedhihirika katika riwaya hizi.Wahusika wa kike wanapinga mitazamo hasi ya wanaume ambayo inalenga kuwagandamiza.Mifano yao ni Sauda na Amina. Wanawake hawa wanapinga ndoa zinazoendelezwa kwa misingi ya mali na za lazima (uk.40a,80b).

### 2.4.2 Harakati za kiuchumi

Kujikomboa kiuchumi kunahusu kuimarika kwa nguvu za kifedha kwa mwanamke ili kuondoa aina yeyote ya kumtegemea mwanamume. Kuimarika kiuchumi huonekana wakati mwanamke anadhibiti nyenzo mbalimbali za uzalishaji kama vile biashara, kilimo na ufugaji pamoja na kuendesha mashirika ya kuzalisha faida. Hali hii humfanya mwanamke kujitegemea kiuchumi.

Mwanamke anaendeleza harakati zake za ukombozi wa kiuchumi kwa kuanzisha miradi mbalimbali ya kiuchumi kama: Mwanaisha na Maria kuanzisha kilimo na ufugaji wa kuku (uk.28b), Dora kuwa mtunzi wa nyimbo (uk.72b) , Amina na Sauda kuanzisha biashara ya duka na *bar (*uk.99a) na Sauda kuanzisha biashara ya mboga (uk.40).

### 2.4.3 Harakati za kisiasa

Harakati za kisiasa zinahusu shughuli ambazo mwanamke anafanya, ili kushiriki katika uongozi. Mwanamke anapigania kupata nyadhifa za uongozi ili kuzima mtazamo hasi wa mwanamume wa kutomshirikisha katika uongozi wa nchi. Viti vya uongozi vinapaswa kutolewa kwa kuzingatia usawa wa kijinsia. Mwanamke amejitambulisha kama kiongozi bora kupitia uongozi wa Mwanaisha. Anapochaguliwa katika bodi ya shule ya Majengo *Academy,* anadhihirisha uwezo wake wa utendakazi. Hatimaye Mwanaisha anachaguliwa kuwaongoza watu katika eneo la uwakilishi bunge la Telek (uk.200).

Harakati za ukombozi wa mwanamke zinachunguza juhudi anazofanya ili kujikomboa kutokana na ugandamizwaji unaomkabili. Dhamira ya harakati za mwanamke ni kumwezesha ajitegemee kisiasa na hivyo kuwa na uwezo wa kupinga dhuluma zinazomkabili kutokana na mwanamume.

## 2.5 Riwaya za John Habwe

Riwaya ya maumble si *Huja na Fumbo La Maisha* ni baadhi tu ya riwaya za Habwe. Mwandishi huyu ameandika riwaya zingine ambazo zina mchango mkubwa wa kimaadili. Riwaya hizi ni: *Maisha Kitendawili*(2000), *Paradiso*(2005) na *Cheche za Moto* (2007).

Riwaya zake ni za kijamii na zinaangazia umuhimu wa kuwa na maadili mema katika jamii. Katika mahojiano naye, Habwe anasisitiza kwamba anatarajia kuwe na jamii

ambayo mwanamke na mwanamume wanaishi pamoja kwa haki, heshima na ushirikiano. Utafiti huu unanuia kudhibitisha ukweli wa madai haya.

### 2.5.1 Muhtasari wa riwaya ya *Maumbile si Huja*

Riwaya ya *Maumbile si Huja* inahusu familia ya kitajiri ya Juma Hamisi na Mkewe Amina ambao ni wa asili ya Kiarabu. Mzee Bilali anaamua kumuoza mwanawe Amina kwa misingi ya Mali. Juma yuko tayari kuwapa shilingi elfu mia mbili kama mahari ya Amina. Ndoa hii inafanywa bila kumhusisha Amina.

Baada ya kumuoa Amina, Juma anaendeleza dhuluma ambazo zinamuathiri Amina kimaisha. Juma anajishughulisha na biashara na kuipuuza jamii yake. Mahusiano kati ya Amina na Juma yanaanza kubadilika, Juma anamdhulumu Amina kwa kumtusi kila kuchao. Uhusiano wao unazorota na Amina anatafuta rafiki anayemjali na kumwonyesha mapenzi ambaye ni Said. Urafiki huu unajitokeza na kuendelea wakati Juma yuko Oman kumtembelea ndugu yake mgonjwa.

Juma anamaliza miezi minane huko Oman na siku zote alizokuwa huko, Amina na Said wanaishi kwake kama mke na mume. Hatimaye wakati Juma unapokaribia kurudi nyumbani, Amina na Said wanafanya mpango wa kuifilisi mali yote ya Juma ambayo ilikuwa nyumbani na hata benki na kuhamia mjini Nairobi.

Juma anaporudi kutoka Oman, anakaribishwa na wafanyikazi wake, Maria na Issa. Anashangazwa kuona kuwa mali yake ya nyumbani imechukuliwa. Anawapigia Polisi

*wa kituo cha Makupa simu ambao wanaandika habari kuhusu kupotea kwa mali hii* Amina anarudi nyumbani baada ya siku kadhaa na katika mahojiano yao Juma, Amina anadai kwamba alikuwa ametoka kidogo kwenda kuwaangalia jamaa zake ambao wanaishi huko Zanzibar. Baada ya majibizano makali, Juma anaamua kukabiliana na Amina kisheria pale mahakamani.

Juma anamshtaki Amina na Said kama watuhumiwa wakuu wanohusika na kupotea kwa mali yake. Siku ya kesi inapofika, Amina na Said wanaachiliwa huru kwa kukosekana ushahidi wa kutosha. Juma anaposhindwa katika kesi hii anaanguka chini na kuzirai. Amina na Said wanarudi Nairobi na kuendelea kuishi katika mtaa wa Buruburu. Ingawa maisha yao yanabadilika kwa kuwa na marafiki wachache, hatimaye hali hii inaimarika.Wanaanzisha biashara ya shughuli za *bar* na duka katika jumba walilokodisha. Biashara hii inastawi na kuwasaidia kujiwekea rasilmali nyingi.

Ghafla katika matangazo ya redio, Juma anaripotiwa kufariki. Amina na Said wanakwenda kujistarehesha katika ufuo wa bahari. Wanafika hadi ufukwe wa *Dolphine* huko Mombasa ambapo wanamzuru mwimbaji wa *MV Slander* Bi. Makopa. Huyu ndiye ameimba nyimbo nyingi zinazomtetea mwanamke kutokana magandamizo ya mwanamume. Amina na Said wanarudi Nairobi na kuendelea na shughuli zao za biashara na malezi. Mungu anawajalia kupata watoto wanne. Watatu wavulana na mmoja msichana.

### 2.5.2 Muhtasari wa riwaya ya *Fumbo la Maisha*

Riwaya ya *Fumbo la Maisha* ni ya John Habwe na imeandikwa mwaka wa 2009. Hii ni riwaya yake ya hivi karibuni kuchapishwa. Kazi hii inahusu maisha ya kijamii na inaonyesha jinsi mwanamke anavyogandamizwa na mwanamume na juhudi anazofanya ili kujikomboa dhidi ya ugandamizi huu.

Riwaya hii inasimulia maisha ya mwanaisha ambaye ni mwana wa Semo Gavalagi kutoka Terek. Mwanaisha ni mwanafunzi wa kidato cha nne katika shule ya *Premier Academy*. Alikuwa na mpenzi wake kwa jina Konya ambaye anampachika mimba. Konya alikuwa ni mwalimu wa shule ya upili ya Vihiga ambaye alifutwa kazi kwa sababu ya ulevi uliozidi.

Mwanaisha anafukuzwa shuleni kwa sababu ya kuwa mjamzito. Anapofika nyumbani, baba yake pia anamfukuza kutoka nyumbani. Mwanaisha anaamua kwenda hadi kwa Konya ambaye ni mpenziwe aliyempachika mimba ili aweze kuchukua jukumu la kumtunza. Konya anampokea Mwanaisha shingo upande lakini mkewe Maria anamkaribisha nyumbani. Konya ambaye ni mwenyeji wake anajisingizia ulevi kama njia ya kumpuuza.

Maria anaendelea kuishi na Mwanaisha huku akimchukua kwa hali zote.Wanawake hawa wanaendelea kushirikiana kuyakabili maisha magumu yaliyokuwa kwa Konya. Maria na Mwanaisha wanaendelea kufanya kazi ya kibarua ili kuikimu familia yao. Maria na Mwanaisha wanaendelea kufanya kazi ya kibarua kama kupalilia mashamba na kuoshea

watu vilima vya nguo kwa malipo ya chini ili kugharamia mahitaji ya familia. Konya anafanikiwa kupata kibarua cha ualimu katika shule ya *Broadways Secondary*. Mshahara anaopata unawasidia kugharamia mahitaji ya maisha, baadaye anabadilika na kuacha ulevi. Kutokana na akiba walizoweka wanaanzisha miradi wa ufugaji wa nguruwe na kilimo cha mboga. Mwanaisha na Maria wanasimamia miradi ya kilimo cha mboga na ufugaji wa nguruwe, kuku na ng'ombe wa maziwa. Mradi wa unaendelea hadi kustawi na kuwapa faida kubwa.

Uhasama wa kikabila kati ya Wanyigu na Wanyuki unalipotiwa kuzuka tena, kwa ;sababu hii miradi ya Mwanaisha na Maria inaangamia. Wanatorokea kambi ya wakimbizi wa ndani kwa ndani kwa kuhofia usalama wao.Familia hii inasambaratika. Maria anakwenda Kisumu na Mwanaisha kupata kazi kwa Doko ambaye alikuwa ]mkurugenzi katika kiwanda cha sukari. Mke wa Doko anamwajiri Susan kazi ya kuwalea watoto wake watatu ambao ni vilema. Kutoka kwa Doko Mwanaisha anapata pesa za kumwezesha kufika Nairobi na kuingia Majengo.Kwa sababu ya mateso maisha yanayo mwandama mwaisha anachagua kuisha Majengo.

Pale Majengo wanashirikiana na wanawake wengine kujiendeleza kwa kuunda mashirika ya kujiinua kimaisha. Wameanzisha biashara, utunzi na uimbaji wa nyimbo na kuwa wanaharaakati wa kupambana na ugonjwa wa Ukimwi. Mwanaisha anakuwa mjamzito na kumzaa mtoto wa kike kwa jina la Husna. Husna anapotimia umri wa kujiunga na shule,anapelekwa katika Shule ya msingi yaMajengo ambapo anafanya mtihani wa darasa la nane na kuibuka mwanafunzi bora kimataifa.

Anakataa kendelea na masomo yake na anakuwa kahaba Hatimaye anaugua ugonjwa wa saratani na kuaaga dunia. Mwanaisha anaamua kurudi nyumbani na kudai haki zake za kijamii na kisiasa. Huko Telek,anaanzisha kituo cha kuuza mafuta ambachomkinastawi na kumpa faida. Anachaguliwa kuwa mwanakamati ya bodi ya shule ya Majengo. Anafaulu katika kazi yake na kuamua kugombea kiti cha ubunge cha Terek. Mwanaisha anapoamua kujiunga na siasa, anaendeleza kampeni zake kwa njia ya amani na utulivu. Anazingatia falsafa ya hayati Mahatma Ghandhi kinyume na siasa za mwanamume zinazojaa chuki na uhasama. Maria ambaye ni mke mwenza anakuja kumpongeza na kuungana naye. Anamhakikishia ushindi katika uchaguzi unaotazamiwa. Hatimaye Mwanaisha anakitwaa kiti cha Terek kutoka mikononi mwa mwanamume. Kwa kuzingatia muhtasari huu tunatarajia kudhibitisha kwamba mwanamke amefaulu kujikomboa katika riwaya ya *Fumbo la Maisha.*

### 2.6 Hitimisho

Katika sura hii ya pili tumetanguliza kwa kutoa maana ya ukombozi wa mwanamke ili kuweka msingi wa uhakiki huu. Aidha tumeonyesha aina mbalimbalimbali za dhuluma zinazomlenga mwanamke. Baadhi ya dhuluma hizi ni: Adhabu kali, kushirikishwa katika ndoa za lazima, kutengewa kazi ngumu, kubaguliwa katika urithi, kubaguliwa katika taasisi za elimu na uongozi. Aidha tumeeleza kuhusu harakati za ukombozi wa mwanamke ambazo ni za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Tumetoa muhtasari wa riwaya ya *Maumbile si Huja* na *Fumbo la Maisha.* Muhtasari wa riwaya hizi mbili unaonyesha jinsi mwanamke anavyodhulumiwa na mwanamume

katika jamii na juhudi mwanamke anafanya ili kujikomboa kutokana na dhuluma hizi. Katika sura ya tatu,tutachunguza ukombozi wa mwanamke katika riwaya ya *Maumbile si Huja.* Aidha tutachunguza njia kadha wa kadha ambazo zinamsadia mwanamke kujikomboa kutokana na dhuluma zinazoelekezwa kwake na mwanamume.

SURA YA TATU

## 3.0. Ukombozi wa mwanamke katika riwaya ya Maumbile Si Huja

### 3.1. Utangulizi

Katika sura ya pili tumeangazia dhuluma zinazomkabili mwanamke kutoka kwa mwamume. Sura hii ya tatu tutaangazia ukombozi wa mwanamke katika riwaya ya *Maumbile si Huja*. Aidha tutachunguza njia kadha wa kadha ambazo zinamsadia mwanamke kujikomboa kutokana na dhuluma hizi.

### 3.2 Ukombozi Wa Mwanamke

Riwaya ya *Maumbile si Huja,* imeangazia jinsi mwanamke anavyogandamizwa na mwanamume. Kwa sababu ya ugandamizi huu maisha ya mwanamke yameathirika pakubwa. Mwanamke amekuwa akilalamika kwa kugandamizwa na mwanamume, mifano ya dhuluma ni kudharauliwa, kubaguliwa, kutukanwa na kupigwa,kushirikishwa katika ndoa za lazima na kutoshirikishwa katika maswala ya kijamii na kiuchumi.

Njia ya pekee ya mwanamke kujikomboa dhidi ya ugandamizi huu ni kupinga juhudi zote za mwanamume zinazolenga kumgandamiza. Wahusika wa kike katika riwaya hii wamejitokeza katika matukio mbalimbali ili kutetea haki zao.Madai ya wanawake kupigania haki zao yanaungwa mkono na Kate Millet (1969:157) ambaye anaeleza kuwa inafaa mabadiliko kamili yafanywe katika mifumo ya kijamii inayomgandamiza mwanamke.Anaweza kutekeleza haya kwa kujiimarisha kijamii, kiuchumi na kisiasa. Harakati hizi zitamuondolea dhuluma ya kutazamwa kama kijakazi, aidha atakuwa huru kiuchumi, kijamii na kisiasa hivi kwamba ataweza kujiamlia mambo yake mwenyewe.

zinazomdunisha mwanamke na kumkuza mwanamume kama vile: ndoa za lazima na kumrithisha mali mwanamume huku zikimbagua mwanamke. Mwanamke anaweza kujikomboa kwa kuwakabili wagandamizaji, kudai haki zao za urithi, kufanya biashara, kukuza vipawa vyao na kudai nyadhifa sawa na wanaume katika uongozi.

### 3.2.1 Asasi za ndoa

wahusika wakuu Amina na Juma katika riwaya ya Maumbile si Huja walioana hawakuishi kwa amani. Maisha yao ya ndoa yalitawaliwa na ugomvi, matusi na madharau. Hali hii ilizua uhasama kati yao na kuishia katika talaka. Haya yanaonekana wazi wakati Amina anamwamsha Said ambaye ni mfanyikazi wao ili amtume dukani kwa Bw. Hussein Mshiri kununua sukari na majani. Juma anaonekana akimshuku Amina kuwa, anafanya mapenzi na mfanyi kazi wao Said. Anamwita na kumzomea:

> "Amina? Amina?"
> ''Naam bwana," Amina akajibu"
> umekwenda kufanya nini huko?
> Tuseme una shughuli na akina Said au vipi?" uk 2.

Unukuu huu unaonyesha jinsi Juma hakumwamini mkewe Amina. Hata bila ya kungalia uzito wa swala la Amina kumtuma Said kuleta sukari na majani. Anamwamuru Amina kumweleza Said kurudi ili amshughulikie kwanza. Juma anaonyesha kutouheshimu uamuzi wa Amina kwa sababu yeye ni mwanamke. Licha ya Juma kumfokea Amina hata

kumtusi. Kabla ya kuanza safari yake ya kwenda Oman kumzuru ndugu yake Agbal, anamtusi Amina. Anamwita:

> "Amina: Amina?.....
> "Huyu mwanamke ni mjeuri sana.
> Sitaki mwanamke mwenye ubongo kama uporo.
> Wanawake wa enzi hizi wamejaa maringo".( Uk 19)

Katika muktadha huu, Amina anadhulumiwa kwa kutukanwa. Juma anaposafiri Oman anakata mawasiliano na mkewe kwa miezi minane. Kiini hasa cha dhuluma hii kinatokana na kwamba, Amina aliolewa na Juma kinyume cha mapenzi yake. Ndoa hii ilipangwa na Bilali babake na Juma bila kumhusisha Amina mwenyewe. Kama njia ya pekee ya kujikomboa Amina anamwacha mumuwe na kujichagulia mume anayemtaka na kumjali. Na kwa sababu jamii anayoishi nayo haitambui juhudi za mwanamke katika kuchangia hazina ya familia, anaamua kuchukua sehemu yake ingawa kwa ulaghai na kuanzisha biashara yake na mume ampendaye(uk.46).

Kama njia ya kujikomboa mwanamke adai uhuru wake wa kumchagua mwanamume anayempenda. Chanzo cha ugomvi wa Amina na Juma ni ukosefu wa mapenzi ya dhati kati yao. Isitoshe kupitia mhusika Suleiman tunaelewa kuwa Juma alikuwa gamba tupu na hii ndiyo sababu kuu ya Amina kumuacha (uk.79). Njia ya kujikomboa kutokana na ugandamizi wa aina hii ni kutengana ili kutoa nafasi bora kwa mwanamke kufanya uamuzi bora kama tunavyoarifiwa katika (uk.60).

Mhusika Sauda analazimizwa na wazazi wake kuolewa na mzee Ramadhani hii ni dhuluma kubwa ambayo inalenga kumbidhaisha mwanamke. Ni muhimu wanawake kuungana katika kupinga hatua zote za wazazi wao kuwaongoza kufanya ndoa za lazima, ili kupata mali ya kuwaelimishia watoto wanaume.Katika riwaya Sauda anaeleza: "Mimi nilikuwa nikisoma katika darasa lanne.mpaka sasa nina umri wa miaka kumi na mitano pekee yake nao wanasema nimebaleghe.Mimi mwenyewe sijui mwalimu mkuu alitufukuza shule kutafuta karo. Mimi na ndugu yangu Hassan tulikwenda nyumbani... Tulipofika nyumbani baba akanieleza eti alitaka kunioza kwa mzee Ramadhan." (Uk.50) Mwanamke ana uhuru wa kujiamlia mwanamume atakayemuoa. Ili kujikomboa inafaa asisitize kupinga dhuluma za ndoa ya lazima. Sauda anaendelea anaeleza :

"Marehemu bibi yangu ningeendeleaje kuishi nyumbani? Baba na Mama walitaka kuniuza kama kitatange sokoni. Mzee Ramadhani alikuja nyumbani akitaka mke wa tatu. Kwa kuwa alitaka kuwapa mali, Mama na Baba walinishurutisha niwe mkewe. Niliamua kukimbia na kuja kufanya biashara...'' (Uk 40)

Mwanamke anapaswa kupinga juhudi zote za kumfanya kama bidhaa ya kuuzwa mnadani ili kugharamia miradi ya nyumbani au masomo ya mwanamume. Tamaduni zinazomshurutisha mwanamke kuolewa na mwanamume ambaye hampendi zimepitwa na wakati. Mwanamke ana haki ya kupinga ndoa zinazofanywa kwa misingi hii na anaweza kufanya hivyo kisheria.

### 3.2.2 Jukumu la malezi

Malezi kwa watoto wa kike ni jukumu la mwanamke. Maadili ya kike hufunzwa na mama. Ingawa Amina anafanikiwa kupata watoto watatu wa kiume, lakini haridhiki na anaendelea kumwomba Mungu amjalie mtoto wa kike, ''Mimi nafikiria kama kweli Maulana atanijalia mtoto wa kike. Akinijalia mtoto huyo basi nitashukuru sana'' (uk.100).

Malezi bora kwa watoto wa kike ni muhimu maana hawa ndio wanaharakati wa kesho ambao watapigania ukombozi kutokana na dhuluma za mwanamume. Kama njia ya kupinga ungandamizwaji ni muhimu akina mana kuwafunza watoto wa kike kujua haki zao ili wachukue mstari wa mbele katika kupinga hali yote ya ugandamizwaji unaowakabili.

### 3.2.3 Mali

Baadhi ya vitu vinavyobainisha, mali ni kama vile: pesa, nyumba, ardhi na bidhaa zilizoekezwa katika biashara. Mali ni nyenzo kuu ya ugandamizaji wa mwanamke. Ili kukabiliana na ugandamizi huu, ni muhimu mwanamke awe na mali yake binafsi. Mali hii itamwezesha kujipangia miradi mbalimbali ya kuzalisha mali zaidi bila kumhusisha mwanamume, ambaye daima hudai kuwa mwenye mali. Amina amepata mali na ndiyo sababu anaweza kuchukua uamuzi wa busara kama anavyosema,

"Fedha ndugu si kitu....(nina) kibunda cha pesa katika benki kwa jina langu.... mashamba mawili kwa jina langu.'' (Uk.47)

Kwa wakati huu Amina na Juma waliishi pamoja kama mke na mume, walishirikiana pamoja kutafuta mali waliyomiliki. Kwa hivyo, Amina kuchukua sehemu ya mali hii kama yake ilikuwa halali. Mali hii ilimsaidia Amina kuishi maisha ya kujitegemea. Kwa kutumia mali aliyopata kwa Juma, alijipatia makao mapya, mahitaji ya familia na kuanzisha biashara.

### 3.2.4 Biashara

Wanawake wengi  wanajiendeleza kibiashara. Katika mjadala kati ya mzee Mgeni na Suleiman wanaeleza kuwa wanawake wengi walikuwa wafanyibiashara ambao waliuuza bidhaa kama dagaa,uduyi, kolekole ,vibua na aina nyingine ya samaki. (uk. 18)

Baada ya kuhama mji wa Mombasa na kuhamia jijini Nairobi. Amina hakukaa kutegemea mali ya wanaume, anaazisha shughuli za kibiashara.

Mwandishi anaeleza:

> "Amina kwa upande wao walikuwa wamekodisha Jumba kubwa lenye vyumba viwili vikubwa. Chumba kimoja kilitumika kwa shughuli za bar na kingine kutumika kwa shughuli za duka". (Uk. 87)

Biashara ya Amina ilistawi na kumsaidia kujiwekea akiba ya benki na mitaji mingine ambayo yangemfaa  katika siku za usoni. Sauda alitorokea mjini Mombasa na kuanzisha biashara ya kuuza mchicha huko Kilifi baada ya wazazi wake kukataa aolewe na mzee Ramadhan ambaye hakumpenda (uk.40). Ingawa biashara hii ilikuwa ya pato la chini, Sauda alitosheka nayo. Alijua uzuri wa kuwa na maisha ya pato la chini kuliko kuwa na

maisha ya utajiri yaliyojaa ugandamizi. Biashara hii ilimsaidia Sauda kujipatia riziki yake kwa kujitegemea.

Kielelezo cha biashara ya Amina na Sauda ni muhimu katika kuleta ukombozi wa mwanamke dhidi ya ugandamizwaji wa mwanamume. Faida iliyotoka kwa biashara ilimsaidia Sauda kujiendeleza kimaisha na itamwezesha kujiwekea akiba ya kuanzisha miradi mingine ya kuzalisha mali. Njia hii itamwezesha mwanamke kujitegemea kiuchumi. Nguvu za kiuchumi ambazo ndizo nguzo kuu za ugandamizaji.

### 3.2.5 Sheria na haki

Mwanamke anapaswa kuelewa sheria na vifungu vyake, ili kuukabili ugandamizwaji wa aina yoyote dhidi yake. Sheria inawapa idhini kupitia katiba kutetea haki zao za usawa mahakamani. Wazo hili linajitokeza wakati Amina anajitetea mahakamani:

> "Kama ni kufuja sijui ina maana gani na sijui ni chini ya kifungu gani cha sheria za nchi hii. Maana Juma aliponioa kulingana na desturi za kidini hakuniambia jinsi ya kutumia mali yake"...
>
> "Kama ni kuiba sielewi. Mimi nikirudi kutoka harusi ya rafiki yangu Hadija Napata Nyumba ishafagiliwa na wezi.Kila kitu kisha kwenda"...(uk.70)

Ingawa Amina hakuwa na wakili wa kumtetea mahakamani sheria iliweza kumtetea katika kesi hii. Juma ana mawakili wengi wa kihindi wa kumtetea mahakamani lakini anashindwa.

Jaji anasema...kwa upande wa Amina tunaona ushahidi wa Maria hauna uhusiano mkubwa wa kuweza kumhusisha. Kwa hivyo tumewaachilia (tumemwachilia) huru(k.h.j)

Ni muhimu mwanamke kuelewa kwamba swala la kulalamikia ugandamizaji bila kuchukua hatua za kusheria halisaidii kupunguza ugandamizi. Katiba ya nchi ya Kenya inaelezea kwamba watu wote ni sawa chini ya sheria na wana haki sawa katika mali na ulinzi( 2009: 3/6/1).

### 3.2.6 Ukuzaji wa vipawa

Kamusi ya TUKI(2004:175) Inaeleza kuwa kipawa ni uwezo ambao binadamu huzaliwa nao . Elimu husaidia kukuza kipawa lakini haiwezi kumpa mtu kipawa. Vipawa hivi ni kama vile: uimbaji, uchoraji, uchongaji,ukimbiaji na vipawa vingine. Vipawa hivi husaidia katika kujipatia riziki. Suala la vipawa limejitokeza na kipawa cha kuimba ambacho kinasaidia kueneza mawazo ya ukombozi wa mwanamke. Anawatumbuiza watu kupitia nyimbo zake ambazo zinawazindua wawake waamke na kutetea haki zao. Katika wimbo mmoja anawazomea wanaume kwa kuwanyima wanawake uhuru (uk. 96).

Nyimbo za Bi. Makopa ni kielelezo kwa wanawake kutambua vipawa vyao na kuvikuza. Vipawa hivi vitawasaidia kuendeleza juhudi zao za ukombozi. mwanamke anapaswa kujitegemea kiuchumi. Kukaa nyumbani na kumngojea mwanamume kumliza ni chanzo cha ugandamizwaji. Mbali na kipawa cha bi Makopa kuna vipawa vingi ambavyo hujitokeza miongoni mwa wanawake , baadhi yao ni usushi na uchoraji .

### 3.2.7 Ushirikiano

Wanawake washirikiane katika kuinua hali zao ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Suala hili linajitokeza kwa wanawake wa Nairobi. Kupitia juhudi zao wanausafisha mji wa Nairobi ilihali mwanamume 'anainua pua lake jeusi lenye tundu ndogo ndogo na kutokomea' (uk.85).

Ni muhimu mwanamke awe mshirika mkuu katika utendakazi. Wanaweza kufanya hivyo kwa kuunda makundi ya wanawake. Hali hii itasaidia kumkomboa mwanamke pamoja na jamii nzima. Ukombozi wa aina hii utamtambua mwanamke kama shujaa na kumuondolea maonevu yote yanayomfanya kudunishwa na mwanamume.

Hata hivyo kuna changamoto kubwa kuhusu ukombozi wa mwanamke. Wanawake wachanga huacha shule na kugeuka kuwa makahaba, hili ni tisho kubwa kwa ukombozi wa mwanamke. Jambo hili linaangaziwa na Sauda anadokeza kuwa wasichana wadogo kama Njeri na Ambiyo wanaacha shule na kuanza kufanya kazi ya ukahaba. Huu ni mwenendo mbaya ambao unaipokonya jamii wanawake ambao wangesaidia katika kupigania haki zao.

## 3.3 Hitimisho

Katika sura hii ya tatu tumeangazia juhudi za mwanamke kujikomboa kutokana na ugandamizi wa mwanamume. Aidha tumechunguza baadhi ya masuala ambayo yanachangia kumgandamiza mwanamke na ambayo anapaswa kuyapinga kama: Asasi za

ndoa, ubidhaishaji wa mwanamke, urithi wa mali, biashara na malezi ya watoto wa kike. Aidha tumeangalia masuala ya sheria na haki, ukuzaji wa vipawa na ushirikiano.

Tumeonyesha namna masuala haya yanavyoweza kuzingatiwa na wanawake katika harakati zao za kujikomboa. Aidha tumeona kwamba pingu za ugandamizwaji zinaweza kuondolewa iwapo wanawake watasimama kidete na kupinga juhudi zote zinazoelekezwa kwao na wale wanaowagandamiza. Juhudi za kujikomboa zinaweza kuwa sahili ikiwa wanamke watajisimamia kiuchumi kwa kufanya biashara, kuwalea wasichana kwa maadili yanayowafaa kama wanaukombozi wa kesho, kudai haki zao za kisheria mahakamani, kushirikiana na wanawake wenzao na kukuza vipawa vyao. Katika sura ya nne tutaangazia juhudi za kujikomboa kwa mwanamke katika riwaya ya *Fumbo la Maisha.*

# SURA YA NNE

## 4.0 Ukombozi wa mwanamke katika riwaya ya *Fumbo la Maisha*

### 4.1 Utangulizi

Katika sura ya tatu tumechunguza ukombozi wa mwanamke katika riwaya ya *Maumbile si Huja.* Sura hii tataangazia juhudi za mwanamke za kujikomboa katika riwaya ya *Fumbo la Maisha.*Aidha tutaonyesha namna mwanamke amefaulu kujikomboa kutokana na dhuluma za mwanamume. Dhuluma hizi ni za kijamii, kiuchumi na kisiasa ambazo zinalenga kumsawiri mwanamke kama kiumbe duni asiye na kwake wala kwao, asiye na mali, asiye na uhuru na kahaba. Ili kuukabili ugandamizi huu mwanamke ameanza harakati zake za kujikomboa, kwa kujiimarisha kijamii, kiuchumi na kisiasa. Ametimiza haya kwa njia mbalimbali kama vile: kupinga juhudi za wagandamizi, kujiendeleza kisiasa na kielimu na kujiimarisha kiuchumi kwa kuanzisha miradi ya kilimo, ufugaji, biashara na harakati zingine za kichumi.

### 4.2 Harakati za ukombozi wa mwanamke

Mwanamke amejitokeza mbele kupinga ugandamizi wa kila aina kwa njia mbalimbali,baadhi ya njia hizi:

#### 4.2.1 Kuwakabili wanaume wagandamizaji

Mpango wa Mwanaisha kusoma hadi kidato cha nne unakatizwa na Konya ambaye anampachika mimba. Jambo hili linasababisha kufukuzwa kwake shuleni. Anapofika nyumbani, babake anamfukuza nyumbani kabla ya kupeleleza ni nani aliyesababisha jambo lenyewe.Anamfokea Mwanaisha:

> "Toka hapa kwangu. Umeamua kuwa mwanamke. Kwa hivyo hapa sikutaki tena....Mwizi! mwizi! Mwizi! shika yeye!shika yeye!"(uk.5)

Mwenye kusababisha mimba ya Mwanaisha ambaye ni mwalimu wake, anakosa kuadhibiwa kwa makosa haya na hata anakataa kuchukua wajibu wake. Mwanaisha anashauriwa na mwanamke mwenzake:

> "Kama unajua (mimba) ni ya nani,nenda nyumbani ujifungue, umpelekee mwenyewe mtoto urudi shuleni"(uk.3).

Mawaidha haya ya mwanamke yanatoa mwanga zaidi wa namna mwanamke anapaswa kukabiliana na dhuluma za mwanamume. Pili,yanadhihirisha wazi kwamba jambo la mwanamke kujikomboa litatokana na mwanamke mwenyewe.

Kwa kuzingatia mawaidha haya, mwanaisha anaikabili dhulima hii kwa kumlazimisha Konya kumuoa kwa kuhamia kwake. Uamuzi huu unamwondolea fedheha kutokana na aibu ya kulea mimba akiwa peke yake ilihali mume aliyehusika yuko huru(uk9).

Uamuzi wa mwalimu mkuu kumfukuza Mwanaisha shuleni kwa kupachikwa mimba hata mwezi mmoja tu kabla ya kufanya mtihani wa kidato cha nne ni aina moja ya dhuluma zinazotekelezwa na mwanamke kwa mwanamke mwenzake. Sheria zinapasa kuwalinda wanafunzi na maslahi yao. Inafaa mwalimu mkuu kwa kushirikiana na wazazi kudadisi

na kumhoji Mwanaisha kuhusu chanzo na mhusika wa mimba yake. Anaamua kumfukuza shuleni bila ya kuzingatia hayo yote.

Ingawa wazazi nao walimfukuza Mwanaisha kutoka nyumbani kutokana na hasira ya mapenzi waliyokuwanayo kwa mtoto wao, hatua yao haifai. Wangempokea Mwanaisha nyumbani baada ya kufukuzwa shuleni na baadaye kudadasi kuhusu kisa chenyewe. Hali hizi zote zinaonyesha jinsi wanawake wanavyodhulumiwa shuleni, vyuoni na hata nyumbani. Wanawake wanafaa kuukabili ugandamizi huu kama njia ya kujinusuru.

### 4.2.2 Kuchukua uamuzi

Mwanaisha aliweza kuyapitia mazingira mbalimbali magumu katika harakati zake za kujikomboa. Maamuzi anayoyachukua yameweza kumfaa kukabiliana na hali mbalimbali za maisha. Hatimaye kupitia maamuzi yake ya busara maisha yake yaliimarika kama inavyojitokeza. Baada ya Mwanaisha kufukuzwa nyumbani na wazazi wake, anachukuwa uamuzi wa kwenda hadi kwa Konya kama anavyeleza:

> "Barua hii ilinitonesha kidonda cha moyo wangu. Nilisikia kulia, niliisoma tena kwa ghibu ilikuwa imeniletea balaa na baba yangu mzazi. Labda hataniona tena. Nilitaka kutokomea mbali. Sikuwa na tamaa ya maisha wakati huu. Sikujua kama alitaka kukumbushwa. Labda akatae. Akikubali akubali…." (uk 6).

Uamuzi huu wa Mwanaisha wa kutoroka hatari ya kuumizwa na babake na kwenda kwa Konya unafaa kwani hakuwa na lingine la kutenda katika mazingira yale kama anavyofafanua:

> "Niliamua kukaa hapo kwa Konya sasa. Nilitaka kuwa mshiriki wa ufuska na umaskini wake. Japo kwa muda sikuwa nimeamua kukaa sasa lakini niliamua kukaa. Maamuzi haya niliyafanya baada ya kipindi kirefu cha kujisaka." (Uk. 21)

Muktadha huu unaonyesha namna ilivyokuwa muhimu kwa Mwanaisha kuchukua hatua hii ili kuepuka majanga yanayomkabili ili kujikomboa. Uamuzi wa Mwanaisha na Maria wa kuanzisha miradi ya kujiinua kiuchumi, uliwasaidia kujiondolea umaskini uliyoitawala familia yao. Aidha baada ya uhasama wa kivita kati ya wanyigu na wanyuki Mwanaisha na maria waliamua kuhamia kambi za wakimbizi wa ndani kwa ndani kama njia moja ya kuepukana na dhuluma za kimapenzi walizozishuhudia pale kambini.

Akiwa majengo Mwanaisha anakabiliana na maisha magumu bila kufa moyo. Alilazimika kuishi maisha ambayo hakuyapenda. Anayaelezea kama maisha yaliyojaa uovu mwingi: "Majengo kulikaa watu ambao tungenyang'anya, tungeua na tungeghilibu. Tungefanya lolote haramu au halali (uk, 104). Kama njia ya kujikomboa kiuchumi, wanawake majengo wanakubali kushirikiana pamoja na kuunda shirika lao la kujiinua kiuchumi la '*The Ten Sisters'*. Shirika hili linawainua kifedha na kuwawezesha kuyakimu maisha yao.

Maisha ya mjini yanapomshinda, anachukua uamuzi wa kurudi nyumbani. Anapofika kwao, Mwanaisha anaanza biashara ya kuuza mafuta kama njia nyingine ya kujikomboa kiuchumi. Biashara hii inastawi na kumpa faida kumbwa na kufaulu kujikomboa kiuchumi. Maria anadhibitisha kwamba wanawake wana uwezo sawa au hata wana uwezo zaidi ya wanaume kwa kuwaajiri wanaume kazi katika biashara yake ya kuuza mafuta. Mwanaisha anadhibitisha ukombozi wa mwanamke kwa kujiingiza katika ulingo wa siasa. Anakiwania kiti cha ubunge cha Telek na kushinda. Uongozi wake wa kisiasa, unadhibitisha uwezo wa wamwanamke kuongoza na hata kuamua masuala ya kijamii kama tunavyoaelezwa na mwandishi:

> "Lazima (mwanasiasa) awe mhimili wa maendeleo, watu na umma.Asiwe mhitaji wa kila namna ya haja ya tumbo lake. tunaafiki kuwa maenndeleo ya mwanamke yanatokana na uamuzi wake mwenyewe anaouchukua kuhusiana na masuala yanayomkabili maishani."(uk190)

### 4.2.3 Mapenzi, umoja na ushirikiano

Baada ya Mwanaisha kufukuzwa nyumbani na wazazi wake, Maria anamkaribisha nyumbani Mwanaisha kama mke mwenza kwa sababu ya mapenzi aliyokuwa nayo. Wanaendelea kuishi pamoja huku wakishirikiana katika kufanya kazi pamoja. Maria anaendelea kufanya kazi ya kibarua ili aweze kukidhi mahitaji ya familia hii yote bila ubaguzi.

Maria alikuwa akiishughulikia familia hii kwa hali na mali, kwa sababu ya mapenzi aliyokuwa nayo. Alielewa matatizo ya Mwanaisha na kuweza kumsaidia kupata mahitaji yake yote kama mzazi. Wanawake hawa waliendelea kushirikiana hata katika kazi za nyumbani na hawakuwahi kukosana. Mwanaisha anaelezea:

> "Mimi na Maria hatujatokea kukosana. Tangu mwanzo hapakuwa na sababu yoyote ya kukosana. Tulishughulika na kunusura roho zetu. Hata baada ya Konya kubadilika tulishikana mikono. Aliniita dada nami hali kadhalika. Kwa kweli tulikuwa kama mtu na mnuna wake. Tuliheshimiana…."(uk 27).

Mapenzi kati ya Mwanaisha na Maria yanawawezesha kukabiliana na hali ngumu ya maisha yaliyokuwa kwa Konya. Ni muhimu wanawake kuelewa kuwa umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu. Inawapasa kushikana mikono ili waweze kupigania ukombozi wao. Upendo, umoja na ushirikiana ni muhimu sana katika kuleta ukombozi wa mwanamke. Inawabidi wanawake waungane katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Muungano huu utawapa nguvu za kutosa za kuukabili ugandamizaji wa aina yoyote. Uhasama na chuki kati ya wanawake hautawasaidia kuleta ukombozi wao.

### 4.2.4. Kilimo na Ufugaji

Udhibiti mwingi wa nguvu za kiuchumi walizo nazo wanaume zinachangia pakubwa katika kumgandamiza mwanamke. Ili wanawake waweze kujikomboa wanapaswa kuanzisha miradi ya kiuchumi kama kilimo na ufugaji. Mwanaisha na Maria wanaanzisha miradi ya kilimo na ufugaji,wanajishughulisha na kilimo cha kabeji, kunde, karoti. Aidha

wanajishughulisha na ufugaji wa kuku, nguruwe na ng'ombe wa maziwa. Mwanaisha anaelezea:

> "Maria .... Alilisha vifaranga, jogoo na koo tangu kucha hadi kuchwe. Mayai yaliyotagwa hapo kwa Konya hayakuhesabika" (uk 28).

Kama njia ya kujikomboa wanawake waanzishe miradi ya kiuchumi ambayo itawawezesha kujiajiri na kujitegemea kiuchumi. Jambo hili litamsaidia katika kusimamia miradi yake ya maendeleo bila kumtegemea mwanamume ambaye humpa masharti magumu yanayolenga kumgandamiza.

### 4.2.5. Mabadiliko

Mkondo wanaouchukua wanawake wa Majengo unaonyesha njia ya ukombozi wao.Wanaacha kumtegemea mwanamume kupitia ukahaba na badala yake wanaanzisha hazina ya pamoja ya kusaidiana. Aidha wanawake hawa wanaonyesha busara na hekima yao kwa kushirikiana kwa kuunda mashirika ya kushughulikia hali yao ya maisha kule Majengo, Mwanaisha anadhibitisha haya:

> "Kikundi chetu kilikuwa cha wanawake kumi. Tulijiita *The Ten Sisters*. Dola alifika mwanzo. Tulimpata akinywa *juice* ya ndimu....tulimchangia shilingi elfu kumi. Tulimnunulia leso mbili. Tulimletea pia na sukari, unga wa chapati, shuka za kitandani na birika zuri la chai" (uk.102)

Ingawa maisha ya majengo yalijaa upotovu wa kimaadili baadhi ya matendo mengine yalikuwa ya manufaa makubwa katika kuwakomboa wanawake pamoja na jamii nzima. Matendo haya ni kama vile: Kuanzisha kampeni dhidi ya ugonjwa wa ukimwi,kuanzisha vyama vya ushirika na kukuza taaluma zao.

**4.2.6 kampeni dhidi ya ukimwi.**

Magonjwa ni kizuizi kikubwa cha ukombozi wa mwanamke. Ugonjwa wa Ukimwi, saratani ya matiti ni baadhi ya magonjwa ambayo yanawaua wanawake wengi majengo ambao wangechangia pakubwa katika kuendeleza harakati za ukombozi wa mwanamke.

Pale majengo Dora anageuka na kuwa mwanaharakati wa kupiga vita ugonjwa wa ukimwi. Anawahamasisha wanawake wote wa majengo kuhusu umuhimu wa kujua hali zao za ukimwi kwa kuwahimiza watu wote wanaojitokeze kupimwa. Anashirikiana na mashirika ya afya kufanya kampeni zake kama tunavyojuzwa:

> ''Dora alipita katika vilango vya watu kupimwa virusi vya ukimwi. Alipopita kwangu alifaa kitambaa kichwani akatia kitambaa cha chepeo chenye maandishi: TAMBUA HALI YAKO YA H.I.V. Dora ni mwanaharakati kweli. Alikuwa na kikundi cha watu waliohimiza kwa nyimbo. Walivaa jesi zenye maandishi ya HIV.''(uk.77)

Aidha Dora anabadilika na kuwa mwimbaji wa kitaifa. Anatunga na kuimba nyimbo za kizalendo siku ya Madaraka na hata kuanzisha duka la kuuza kanda.

Mkondo anaouchukua Dora, ni njia moja ya wanawake kujikomboa na kuikomboa jamii nzima. Juhudi za Dora kuwahamasisha wanawake wenzake kuishi kizalendo kupitia nyimbo zake kunasaidia kupunguza hatari ya wanawake kuangamia kutokana na ugonjwa wa ukimwi. Mwanamke huyu anaendeleza harakati za ukombozi wao.

**4. 2.7 Kuanzisha vyama vya ushirika.**

Vyama vya ushirika huwasaidia wanawake kujiendeleza kiuchumi. Pale Majengo wanawake wanaanzisha chama chao cha mzunguko cha 'The ten sisters'. Chama hiki kilinuia kuwaunganisha wanawake ili waweze kujiinua kiuchumi. Chama hiki kilikuwa na idadi ya wanawake kumi ambao walikutana kwa zamu kila Jumamosi nyumbani mwa kila mwanachama ili kuchanga fedha za kujisaidia kama Mwanaisha anavyoeleza,

> "Kikundi chetu kilikuwa cha wanawake kumi. Tilijiita '*The ten sisters'*. Dora alifika mwanzo, tulimpata anakunywa *juice* ya ndimu. Hii tena ilikuwa siku ya Selume, tulimchangia shilingi elfu kumi. Tulimnunulia leso mbili, tulimletea pia na sukari, unga wa chapati shuka za kitandani na birika zuri la chai." (uk 102)

Ingawa chama hiki kiliwajumlisha wanawake wa Majengo pekee, bado ni kielelezo bora kwa wanawake wote kuhusu ukombozi wao kiuchumi. Badala yao kuwategemea wanaume, wanawake wanapaswa kujitegemea kiuchumi kwa kuiga juhudi za wanawake wa majengo.

Michango waliyopata kwa ushirikiano wao iliweza kuwasaidia kijiendeleza kimaisha. Wengine walianzisha biashara na wengine kuwalipia watoto wao karo. Mtazamo kuwa mwanamke ni kahaba ni matokeo ya jamii ambayo huwa na mtazamo hasi kumhusu mwanamke. Mtazamo unadhihirika wazi tunapogundua kwamba neno 'kahaba' halipo miongoni mwa wanaume wanaoogelea katika bahari hii.

### 4.2.8 Kukuza taaluma zao

Pale Majengo wanawake waliweza kujitegemea kwa taaluma walizokuwa wamejifunza hapo awali. Baadhi ya taaluma hizi ni ufumaji na upishi. Taaluma hizi zinawasaidia kujipatia riziki kama njia ya kujikomboa kiuchumi.

Mwanaisha anaendeleza kazi yake ya ufumaji wa vitambaa ambavyo anaviuza na kujipatia pesa. Selume naye anapika vitumbua, viazi karai, sambusa kubwa, mandazi, chapati, biriani na pilau ambavyo aliviuza na kujipatia riziki yake (uk.83). Hizi ni njia zingine za kujikomboa kiuchumi. Ni muhimu mwanamke kujifunza taaluma mbalimbali kama mwongozo wa kutekeleza kazi anazokabiliana nazo maishani.

Ili mwanamke aweze kujitegemea kiuchumi inambidi kubadilisha hali yake ya maisha kwa kuanzisha mradi wowote ambao utamsaidia kujipatia riziki yake bila kumtegmea mwanamume. Kwa hivyo ni jukumu la mwanamke kujifuza taaluma yoyote ile ili kujikomboa kutokana na dhuluma za mwanamume.

### 4.2.9. Biashara

Biashara imechukua nafasi kubwa kwa ukombozi wa mwanamke katika riwaya ya *Fumbo la Maisha* . Wahusika wengi wanajishughuliza na biashara. Baadhi yao ni kama Mwanaisha, Selume na Dora.

Kugandamizwa kwa wanawake kunaweza tu kufikia kikomo iwapo wanawake watashiriki katika mifumo inayohimiza maendeleo ya kiuchumi (Sweetman 2000:2). Biashara ni njia moja kuu ya kumwendeleza mwanamke kiuchumi. Hii ni kwa sababu mifumo mingi ya kijamii inampa mwanamume haki ya kumiliki mali yote ya familia na kumtenga mwanamke.

Dora anajishughulisha na biashara ya kuuza kanda za muziki pale Majengo. Mwandishi anaeleza kuwa Dora alikuwa na kiduka cha muziki. Aliuza *CD.ROM*...(uk.59)
Baada ya Mwanaisha kurudi nyumbani Telek, anaanzisha biashara ya kuuza mafuta kwa kutumia rasilmali alizokuwa nazo. Biashara hii inastawi sana na kumletea faida nyingi. Mwanaisha anasema:

> "Biashara yangu ya mafuta ilifana. Kituo changu nilichokianzisha kilivuma hapo kwelikweli. Hapo kituoni kuliitwa kwa Mwanaisha. Hapo kutuoni nilianza kuyakarabati maisha yangu ambayo yaliraruka viraka viraka." (uk. 188)

Biashara ya Mwanaisha ni muhimu kwa wanawake wote kama kielelezo cha njia ya kujikomboa kiuchumi. Inambidi mwanamke atambue miradi ya kiuchumi inayomfaa

kujiendeleza kimaisha. Njia nzuri ya mwanamke kufikia lengo hili ni kuanzisha biashara kwa kutumia rasilmali zilizoko kama vile; Kuuza mafuta, nafaka, mafuta ya kupikia, mavazi, vinywaji na bidhaa nyingine za viwandani.

### 4.2.10 Kudai haki.

Mwanamke amegandamizwa pakubwa kupitia vyombo vya ugandamizi ambavyo ni utamaduni na ndoa. Mwanamke amelelewa akijua kwamba mali yote imo mikono mwa mwanamume. Mwanaisha anapata wakati mgumu anaporudi nyumbani na kuanza kudai urithi wake kutoka kwa wazazi. Anapata ugumu wa kufikia mali yoyote kwa sababu yeye ni mwanamke.

Sheria za kitamaduni hazikumruhusu mwanamke kupewa ardhi nyumbani kwao. Mwandishi anaeleza kuwa, mwanaisha alipata ugumu wa kupata mali kwa ndugu zake kwa sababu ya utamaduni. Mwanamke hakuruhusiwa kupata ardhi nyumbani kwao. Tunaambiwa:

> "Mama hakuwa msemaji sana. Hapo nyumbani hakuwa na chake. Kila kitu; shamba, ng'ombe " (uk. 188).
>
> Isitoshe wanawake wananyimwa haki zao pale Majengo anavyolalamika Dora.Anadai jengo la *Ngolosho Towers* ambalo wamenyang'anywa na matajiri. Mradi ambao ulikuwa miliki ya wanawake wa Majengo (uk.81)

Katika mazingira haya, tunaona namna wanawake wanapata ugumu katika kurithi mali ya wazazi wao. Watoto wanaume hudai kuwa warithi wa pekee na kuwatenga watoto kike jambo ambalo linaloendeleza ugandamizi. Ili kupata ukombozi wa wanawake, ni muhimu mwanamke aendelee kudai haki yake kwa sababu sheria inamruhusu kufanya hivyo. Kando na urithi Mwanaisha anadai haki yake kwa wazee ya kuwania kiti cha ubunge cha Telek. Ingawa alipata pingamizi kubwa hatimaye anakubaliwa na wazee waposema:

"Mwanetu...tunaona tukupe nafasi ya kupigania kiti hiki ili sisi nasi Wanyuki tuwe na mtu wetu huku juu"(uk.189).

Katika muktadha huu, Wanyuki hatimaye wanatambua uwezo wa Mwanamke wa kuongoza jamii sawa na mwanamume. Ukombozi wa mwanamke unaweza kupatikana iwapo mwanamke ataendelea kudai haki zake hadi pale atakapoipata. Morgan (1992:78) akimnukuu Beauvoir (1949) anasema, "Nina hakika huwa mabadiliko anayodai mwanamke hatimaye atayapata."Mwanaisha anadhibitisha maoni haya anapokinyakua kiti cha Ubunge cha Telek (uk.200).

### 4.2.11 Elimu

Elimu ina mchango mkubwa katika maisha ya mwanamke. Maarifa wanayopata katika elimu huwasaidia kukabiliana na hali mbalimbali za kimaisha. Elimu inayoyopatikana shuleni humsaidia mtu kukua kiakili, kuwa na mtazamo wa mbali , kukua kimaadili, kutambua haki zao na hivyo kupinga aina yote ya ugandamizaji.

Ingawa Mwanaisha hakuweza kufanya mtihani wake wa kidato cha nne kwa sababu ya udhalimu aliotendewa na Konya. Maarifa aliyoyapata shuleni yaliweza kumsaidia kukabiliana na hali ngumu za kimaisha. Alikuwa ni mwanamke mwenye maarifa mengi ya kujiendeleza kimaisha. Kwa kuongezea tajriba ya kimaisha aliyopata kwa kukulia katika mazingira mbalimbali.

Walianzisha miradi ya kiuchumi ambayo ilifaulu pakubwa. Baadhi ya miradi hii ni kama vile kilimo na ufugaji, biashara na kujiendeleza kisiasa. Lengo kuu la kuanzisha miradi hii lilikuwa ni kujitegemea kiuchumi kama njia ya kuukabili ugandamizaji wa wanamume. Umuhimu wa elimu unaoneka katika maisha ya Hasna. Kijana huyu mwanamke alisomea katika shule ya majengo na akaweza kuibuka mmoja wa wanafunzi kumi bora katika mtihani wa kitaifa wa darasa la nane. Mwandishi anasema:

> "Kweli Husna ...alipita akawa mwanafunzi katika kumi bora. Magazeti yalichukua picha zake. Yakamtangaza. Maisha ya aluwa sasa yalifunuka mbele yake. Aliitwa katika shule ya Aliance Girls" (uk .123).

Ingawa alipata matokeo mema, Husna anakataa kuendelea na maomo yake, matokeo yake ni kwamba anajiingiza katika maovu ya kijamii kama ukahaba na ulaghai kama njia ya kujikimu kimaisha. Mwishowe anaugua na kufa kifo cha aibu.

### 4.2.12 Siasa

Wanawake wa Majengo wa Majengo wanashiriki katika siasa, baadhi yao ni Dora na Mwanaisha. Dora alikuwa mwanaharakati wa siasa za Majimbo katika eneo bunge la Majengo.(uk.86) Suala la kuwajumuisha wanawake katika siasa ni muhimu. Wanawake wamebaguliwa katika uongozi (Sweetman 2000:3). Maendeleo ya kiuchumi ambayo ni ya haki na ya kudumu hutegemea uhuru aliopewa mwanamke katika uongozi wa kijamii. Uwezo wa kuongoza umo katika jinsia zote, suala la kuongozwa na jinsia ya kiume pekee halipo tunapozingatia haki bali ni aina ya ugandamizaji.

Mwanaisha anapata upinzani mkubwa kwa kushiriki katika siasa. Anavumilia na kuendelea na kampeni zake kwa njia ya amani dhidi ya mpinzani wake Bw. Kimera. Maono yake kujiunga na siasa si suala linalotokea kisadfa, alijifunza siasa alipokuwa Majengo, akiwa mfuasi wa Mhe. Kiwembe (uk.86) Isitoshe Mwanaisha alipohamia Telek, alichanguliwa kufanya kazi katika bodi ya Majengo Academy. Kwa sababu ya kazi nzuri na mchango wake mkubwa katika sekta ya elimu na ya kijamii kama matanga, arusi na dini. Mwanaisha anadhibitisha ukombozi wa mwanamke kiuchumi, kisisa na kijamii. Anaeleza:

> "Nilitaka kuwa mwaminifu tu kama nilivyowahudumia kwenye bodi za shule, kwenye harambee ni hivyo hivyo, niliyavulia nguo maji.Nilijiweka tayari kuyaoga bila usiri bila kulimatia, nayo ilitaka kujitolea mhanga…." (uk. 190.)

Maisha ya Mwanaisha katika siasa ni kielelezo kwa wanawake kwamba ukombozi wa mwanamke si ndoto lakini ni jambo la kihalisia. Ili kukabiliana na ugandamizaji wowote ule, aidha ni wa kichumi, kijamii au kisiasa, mwanamke anapaswa kuwa mstari wa mbele ili kudai na kupigania zake katika jamii. Katika riwaya ya Fumbo la Maisha Mwanamke amejitokeza na sifa nyingi zinazodhibitisha kwamba amejikomboa kutokana na ugandamizi wa mwanamume. Baadhi ya sifa hizi ni :

Mwanamke amejitambulisha kupitia utendakazi bora, unaozingatia haki na uaminifu kwamba ana uwezo sawa na mwanamume wa kuiongoza jamii kufikia mafanikio makubwa. Kuchaguliwa kwa Mwanaisha kama mbunge kunadhihirisha kwamba hata mwanamume ametambua uwezo wa mwanamke wa kuongoza jamii. Uongozi wa mwanamke uanajitokeza kama wenye utu, uvumilivu na maono ya mbali kama Mwanaisha anavyosema:

> "lazima mwanasiasa awe mtumishi. Lazima awe mtu wa kuaminika. Lazima awe mhimili wa maendeleo, watu na umma. Asiwe mhitaji wa kila namna ya haja ya tumbo lake."(uk.190)

Mwanamke ameonyesha uwezo wake wa kujikomboa kichumi kwa kuungana pamoja ili kuyatatua matatizo yao bila kumhusisha mwanamume katika uamuzi huu. Aidha amejikomboa kiuchumi kwa kuanzisha miradi ya vitega uchumi inayomletea faida kubwa inayomwezesha hata kumwajiri mwanamume. Ukombozi wa mwanamke kiuchumi unakuwa msaada mkubwa kwa jamii nzima na kudhibitisha msemo kwamba 'kumkomboa mwanamke kiuchumi, kisiasa na kijamii ni sawa na kuikomboa jamii

nzima lakini kumkomboa mwanamume,ni sawa na kumkomboa mtu binafsi.'Mwanaisha anadhibitisha madai haya:

> "Mama alijaa tabasamu usoni.Aliniona na tumaini kidogo.Watu wa kwetu wakawa hawaoni haya ya kutafuta msaada wa usaidizi kutoka kwangu. Na mimi sikusita kuwasaidia. Nilipa karo,nililipa gharama ya hospitali,niliwanunulia watu chakula....Mkewe ambaye hakuwa na kazi akawa na kazi akawa ndiye msaidizi wangu mkuu hapo kituoni" (uk.189).

Kwa kuzingatia nadharia yetu ya ufeministi wa kirasimi tumebainisha wazi kuwa mwanamke katika riwaya *ya Fumbo la Maisha* , amefaulu katika kupinga hali zote za mwanamume kumgandamiza.Ametekeleza haya kwa kujiimarisha kijamii, kiuchumi na kisiasa.

### 4.3 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili kuhusu harakati za mwanamke za kujikomboa kutokana na ugandamizaji wa mwanamume. Tumeona kuwa ili harakati za mwanamke ziweze kufanikiwa ni muhimu mwanamke kuchukua msitari wa mbele katika ukombozi huu. Ilikujikomboa mwanamke amefanya juhudi kubwa kupinga ugandamizaji unaoumkabili. Amefanya hivyo kwa kujiimarisha katika nyanja ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Ametimiza haya kwa kuanzisha miradi ya kilimo na ufugaji , biashara ,kuingia katika siasa za uongozi wa jamii yake. Aidha mwanamke amejiendeleza kielimu na kushirikiana na mwanamke mwenzake kuanzisha mashirika ya kujisaidia. Hatimaye amejifunza

taaluma mbalimbali ambazo zimemwezesha kukabiliana na changamoto za maisha.Azma kuu ya harakati hizi ni kumfanya mwanamke ajikomboe kiuchumi, kijamii na kisiasa. Suala ambalo limetimia kwa kiasi kikubwa kupitia riwaya za Habwe:*Maumbile si Huja* na *Fumbo la Maisha*.

# SURA YA TANO

## 5.0 Hitimisho

### 5.1 Utangulizi

Katika utafiti huu, madhumuni yetu yalikuwa ni kuchunguza ukombozi wa mwanamke katika riwaya mbili za Hawe:*Maumbile si Huja* na *Fumbo la Maisha.*

Tumechunguza jitihada za mwanamke za kujikomboa kutokana na dhuluma za mwanamume katika jamii. Lengo letu hasa lilikuwa ni kuonyesha juhudi anazofanya mwanamke katika harakati za kujikomboa kutokana na ugandamizaji wa mwanamume.

Katika riwaya za Habwe tumejadili dhuluma zinazomkabili mwanamke na harakati mbalimbali anazofanya ili kujikomboa kutokana na dhuluma hizi za mwanamume. Aidha tumejadili jitihada anazopitia mwanamke katika harakati za kujikomboa na hatimaye namna anavyofanikiwa kujikomboa.

Katika utafiti huu tumeongozwa na nadharia ya ufeministi wa kirasimi. Aidha tumethibitisha kwamba nadharia; hii inaafiki kuchunguza suala la ukombozi wa mwanamke katika riwaya za *Maumbile si Huja* na *Fumbo la maisha.*

Katika utafiti huu, tumeona kwamba ukombozi wa mwanamke unamtegemea mwanamke mwenyewe. Mwanamke anafaa kuchukua mstari wa mbele ili kupigania haki zake za kijamii kama njia ya kupinga ugandamizwaji anaotendewa na mwanamume. Ili kutimiza haya inafaa mwanamke ajikomboe katika hali zote za maisha kama vile: kijamii, kiuchumi na kisiasa. Anapofikia hali hii, mwanamke ataweze kujitegemea katika utendakazi na kuchukua uamuzi wa

busara katika jamii. Kufanya hivi kutaweza kumwondolea majaribio yanayolenga kumgandamiza. Katika utafiti huu tumeweza kuonyesha namna wahusika wa kike katika riwaya za Habwe wamejishughulisha na harakati mbalimbali zinazolenga kuwakomboa kutokana na ugandamizaji wa wanaume.

Katika sura ya pili tumeweza kutaja baadhi ya riwaya zingine za mwandishi ambazo kwa ujumla zinanuia kuleta heshima, haki, usawa na ushirikiano katika jimii. Aidha tumeweza kujadili hali mbalimbali za ukombozi wa kijamii, kiuchumi na kisiasa. Tumejadili kuhusu dhuluma wanazopitia wanawake kutoka kwa wanaume. Baadhi ya dhuluma hizi ni: kupewa adhabu kali, kulazimishwa katika ndoa, kubaguliwa katika urithi, kubaguliwa katika taasisi za elimu na kubaguliwa katika uongozi. Ugandamizaji huu hutekelezwa na vyombo vya kijamii kama vile: Utamaduni ndoa na dini.

Katika sura ya tatu na ya nne tumejadili kuhusu harakati za kujikomboa dhidi ya dhuluma za mwanaume. Kupitia riwaya ya *Maumble si Huja.* Tumeonyesha namna mwanamke amejiimarisha kiuchumi na kijamii lakini kwa kiasi kikubwa kwa kutegemea nguvu za mwanamume. Riwaya hii imeonyesha mwanzo tu wa harakati za ukombozi ambapo mwanamke amejikomboa kwa kiasi kidogo.

Kwa kutumia mali ya mwanamume, mwanamke amejianzishia miradi ambayo imefanikiwa kwa kiasi kidogo. Mwanzo huu umekuwa msingi wa ukombozi wa mwanamke ambao umetimizwa na riwaya ya pili Katika riwaya ya *Fumbo la Maisha,* mwanamke ameweza kujikomboa kiuchumi, kijamii na kisiasa. Hali hii imethihirika wazi kwa sababu mwanamke amekwisha

anzisha miradi yake ya kiuchumi kama vile biashara, kilimo, na ufugaji ambayo inalenga kumfanya ajitegemee. vilevile amedai na kupewa haki zake kama vile ardhi na nafasi za uongozi na hivyo kuchaguliwa kuwa kiongozi wa kisiasa.Hizi ni juhudi kubwa ambazo zinamuondolea mwanamke dhuluma ambazo zinamkabili.

## 5.2 Upimaji wa Nadharia

Tumeweza kutumia nadharia ya ufeministi wa kirasmi. Ufeministi huu umejifunga kwenye kipindi cha wakati wa mwanzo kabisa ambacho kilizinduliwa na waasisi wa dhana ya ufeministi ambayo ilipigania haki za wanawake.Ufeministi umekuja kufungamanishwa na wakati na kuwa nadharia ya ufeministi wa Kirasimi.Nadharia hii imetufaa katika utafiti huu kwa sababu baadhi ya masuala anayolalamikia mwanamke kugandamizwa kwayo na mwanamume bado ni yale yaliyotokea nyakati za Karl Marx.Kwa sababu hii nadharia hii imetufaa kuhakiki mada yetu ya ukombozi wa mwanamke katika riwaya za Habwe: *Maumbile si Huja (*1995*)* na *Fumbo la Maisha(*2008).

Kwa kuangazia harakati mbalibali ambazo mwanamke anatekeleza, tumefaulu kuonyesha kwamba mwanamke ameweza kujikomboa kiuchumi, kisiasa na kijamii. Wahusika wa kike katika riwaya ya *Fumbo la Maisha* sasa wanajitegemea katika kujiendeleza kimaisha. Wanamiliki ardhi, biashara na wana uhuru wa kuwania nyadhifa kuu serikalini.

Aidha tumedhibitisha kwamba, utamaduni ndicho kizingiti kikubwa kinachotatiza juhudi za mwanamke za kujikomboa. Mwisho tumeonyesha kwamba nadharia yetu ya ufeministi wa kirasimi imefaulu kuzihakiki riwaya za Habwe.

### 5.3 Mapendekezo

Utafiti huu unahusu ukombozi wa mwanamke katika riwaya mbili za Habwe *Fumbo la Maisha* na *Maumbile si Huja*. Katika utafiti huu tumekumbana na shughuli za mwanamume kumkomboa mwanamke baadhi yao ikiwa ni kumpa mwanamke ulinzi, msaadawa pesa na wa kijamii.Lakini kwa sababu haja yetu ilikuwa ni kuonyesa jinsi mwanamke anavyojikomboa katika riwaya zetu za utafiti tunapendekeza utafiti mwingine kufanywa kuhusu umuhimu wa mwanamume katika ukombozi wa mwanamke. Aidha utafiti zaidi unaweza kufanywa kwa kuangazia mwingiliano wa fani na maudhui katika riwaya ya *Fumbo la Maisha* na *Maumbile si Huja.*

## MAREJELEO


Beauvior, S. (1949), *The second Sex*. London: Pan Books Ltd.

Browne, J.(2007) *The Future of Gender*. New York: Cambridge University Press,

Dorithy,A. (2007) A Critical Analysis of Partriachy and Masculinity in Kezelahabi's *Rosa Mistika na Kichwamaji*. Tasnifu ya uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapichwa

Eagleton, M. (1991:7) *Feminine Literary Criticism* . London: Longman Group Limited

Habwe, J. (2009), *Fumbo La Maisha*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation

..............(1995) *Maumbile si Huja*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation

*Katiba ya Nchi ya Kenya* (2009).Nairobi :Toleo la Serikali.

Lugano, R. (1989) Mwanamke Katika Riwaya za Kezilahabi. Tasnifu ya M.A. chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa

Majumdar, S. (1953) *Great Women of India*. Himalayas: Mayarat Almora

Mbatiah,M. (2001) *Kamusi ya Fasihi*.Nairobi: Standard Textbooks Graphics and publishing.

............(1997) The Origin and development of the Swahili thesis novel in Tanzania.Tasnifu ya PhD.Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Millet, K. (1969) *Sexual Politics* . Newyork: Doubleday & Company.

Moi, T. (1985) *Sexual / Textual Politics. Feminist Literary Theory*. London: Routledge

Morgan, R. (1992) *The World of a Woman*.New York: Norton And Company.

Mugambi,E.(1983) Kilio Cha Wa Nyonge katika riwaya za Said Ahmed Mohamed. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Ndungo, C. (1985) 'Wanawake na mabadiliko ya kihistoria katika fasihi ya Kiswahili'. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa

Okemwa, C. (2008) Mashida's Cooking pot. Acreative Exploration of Women Issues in Kenya. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa

Porter,G.(2002) *Balancing the Local: Gender and Transport*, London Zedbooks Ltd.

Robert, S.(1968) *Uutubora Mkulima*. London: Nelson.

.............(1968) *Siku ya Watenzi* Wote.London: Nelson.

Rutere,M.(1990) Patriarchy and Masclinity in Ngugi's Novels thesis.University of Nairobi.Unpublished.

Stanford, S.(1998) *Mappings and The Cultural Geographies of Encounter*. Princeton: Princeton University Press.

Sojourner,T. (1851) *The Changing Woman* Free Encyclopedia.

Sweetman, C. (2000) *Women and Leadership*. Banbury: Oxfum .

TUKI (2006) *English – Swahili Dictionary* 3rd Edition.Dar es salaam: Institute of Kiswahili Research.

Walibora,K. (2006) *Siku Njema*.Nairobi: Longhorn Publishers Kenya Ltd

Wamitila, K.(1999) *Nguvu ya Sala*.Nairobi:Phoinix PublishersLtd.

................(2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake.* . Nairobi: Phoenix publishers Ltd.

.....................(2003) *Kamusi ya Fasihi: Istlahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publications Ltd

......................(2006) *Msimu wa Vipeopeo*. Nairobi: Video-Muwa.